# Nipashe

Jumanne Juni 25, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581718

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**KANE AJIBU SHUTUMA UCHEZAJI DUNI ENGLAND**

UKURASA 21

**Mfanyakazi** TANAPA na familia yake wazikwa

UKURASA 4



**'Kliniki ya Makonda'** Rais Samia aagiza wenye magonjwa makubwa wapelekwe hospitali za serikali

UKURASA 5



**Maandamano** Kenya, Rais Ruto atoa neno

RAIS wa Kenya, William Ruto, amesema kwamba yuko tayari kufanya mazungumzo ...

UKURASA 19



## MGOMO WAFANYABIASHARA

# Serikali yasitisha ukaguzi risiti EFD

UKURASA 2

## Mwinyi akataa kuongezewa muda u-Rais

UK. 3

UKURASA 2

## Mbowe asema mwakani ni mpambano CDM na CCM





Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (wa pili kushoto) na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, wakizungumza na viongozi wa wafanyabiashara baada ya kumalizika kwa kikao chao jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** YANGA SC YAISUBIRI SIMBA DILI LA CHAMA UK.24

**MAONI,** UK.6



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiongoza kikao cha kawaida cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM Zanzibar, kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui Wilaya ya Mjini Unguja jijini Zanzibar jana. **Habari kamili Uk.3** **PICHA: IKULU**

# Serikali yasitisha ukaguzi risiti EFD, ritani za kodi

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesitisha ukaguzi wa risiti za kielektroniki na ritani za kodi iliyokuwa ikifanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupitia mkoa wa kikodi Kariakoo na maduka kufunguliwa jana.

Baadhi ya wafanyabiashara waliozungumza na Nipashe waliokutwa wameketi nje ya maduka yao walisema walilazimika kutii agizo la viongozi wao la kufunga biashara ili changamoto wanazotaka zitatuliwe.

Mmoja wa wafanyabiashara wadogo aliyejitambulisha kwa jina moja la Fortunatus, alisema wanaendelea na biashara, lakini kwa jana haikuwa nzuri kama ilivyo siku zote.

"Yaani ni bora wafanyabiashara wafungue maduka yao, kwa sababu imetuathiri na sisi, wanunuzi wengi hawajafika leo kwa sababu wamesikia kuna mgomo kwa hiyo na hata kwetu biashara ni ngumu, hatujazoea namna hii," alisema.

Nipashe lilishuhudia baadhi ya wafanyabiashara wakiuza bidhaa kwa kufungua na kufunga maduka yao wakihofia wasigundulike kukiuka taarifa waliyopewa na viongozi wao.

"Yaani hapa tunachofanya hasa kwa wateja wetu wakubwa ili tusiwapoteze, wakija, unafungua anaingia dukani halafu unafunga mlango huku biashara ikiendelea ndani...na tumefanya hivi sana, hivi unafikiri utafanyaje, mteja ametoka mbali, amelipa nauli yake halafu usimuuzie...haiwezekani, kikubwa uhakikishe geti haliko wazi," alisema mmoja wa wafanyabiashara katika eneo hilo la Kariakoo.

Wengine waliolalamika kukumbwa na athari iliyotokana na mgomo huo ni wachuuzi wa bidhaa kama matunda, nyanya, mboga na mamalishe, kwamba kutokana na idadi ndogo ya wanunuzi, mauzo hayakuwa mazuri kwao.

Baadhi ya wanunuzi ambao walizungumza na Nipashe akiwamo mkazi wa Gongolamboto, Agnes Martin, alisema ni vema serikali ikamalizana na changamoto za wafanyabiashara hao ili isiwe jambo la kujirudia kila wakati.

**UKAGUZI WASITISHWA**

Wakati mgomo huo ukishika kasi, mkoani Dodoma kikao kilichofanyika baina ya serikali na viongozi wa wafanyabiashara kilitaja mambo sita yaliyofikiwa ni uamuzi wa kusitisha ukaguzi wa risiti za kielektroniki na ritani za kodi iliyokuwa ikifanywa na TRA.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, ndiye aliyetoa maazimio ya kikao hicho na kueleza kuwa utaratibu huo umesitishwa na unaandaliwa mzuri wa utekelezaji wa suala hilo.

Prof. Mkumbo alisema mwezi Julai, TRA itapitia upya mfumo wa nyaraka ili kupata ukadiriaji sahihi na operesheni za kamata kamata ambazo ilikuwa inafanya mamlaka hiyo zimesitishwa.

Alisema suala la ukokotoaji wa kodi ni la kisheria, hivyo serikali inaendelea kuliangalia.

Kadhalika alisema serikali imewahakikisha itaendelea kuwapanga machinga kama Rais Samia Suluhu Hassan alivyoagiza ili wasiingiliane na wenye maduka.

"Tumewaeleza kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha 2024 bado haujapitishwa na Bunge na kwa sasa wanaita makundi mbalimbali kutoa maoni, hivyo tumewataka nao wapeleke maoni yao ili yafanyiwe kazi kabla haujapitishwa," alisema.

Prof. Mkumbo alitaja jambo lingine ni kuhusu kamati ya Waziri Mkuu ambayo ilibuka na changamoto 41 na kati ya hizo, 35 zikihusu mambo ya utendaji na sita kuhusu sheria na sera, ambapo zote zinafanyiwa kazi.

Wengine waliohudhuria kikao hicho kilichoongozwa na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba ni taasisi zinazosimamia masuala ya wafanyabiashara na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji na viongozi wengine waandamizi wa serikali.

**WABUNGE WAHOJI**

Baadhi ya wabunge jana walihoji na kutaka kupata majibu kutoka serikalini kuhusu mgomo wa wafanyabiashara hao.

Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma, aliomba mwongozo bungeni kuhusu sakata hilo akitaka kauli ya serikali baada ya wafanyabiashara hao kufunga maduka eneo la Kariakoo.

"Mheshimiwa Naibu Spika kumekuwa na kipeperushi kinatembea mitandao kuanzia siku ya Ijumaa, Jumamosi, Jumapili kuwa Jumatatu (jana) wafanyabiashara watafunga maduka ambayo ni leo (jana) na tunapozungumza sasa hivi Kariakoo imefungwa hakufanyiki biashara".

Aliomba kupata kauli ya serikali kulingana na kinachoendelea eneo la Kariakoo, akitoa mfano wa watu wanatoka vijijini wanaokwenda jijini Dar es Saalam kufuata mahitaji na kukuta maduka yamefungwa.

Alisema baadhi ya watu hao wengi wao hawana pesa za kujikimu ikiwamo kulala jijini Dar es Salaam kwa sababu walitarajia kupata huduma na kurudi mikoani mwao.

Musukuma alisema baadhi ya watu wameanza kuwaomba fedha wabunge, hivyo aliomba mwongozo wa Naibu Spika akitaja kufahamu nini kauli ya serikali kukuhusiana na wafanyabiashara waliofunga maduka hayo.

Akijibu mwongozo huo, Naibu Spika, Mussa Zungu, alisema tangu juzi na jana viongozi wa serikali na wafanyabiashara wamekutana na taarifa rasmi kuhusu suala hilo zitatolewa baada ya kikao hicho kumalizika.

"Mheshimiwa Musukuma juzi kwenye mchango wako ulizungumzia hoja hii na juzi na jana viongozi wa serikali na wafanyabiashara wamekuta, taarifa rasmi ya serikali tutaipata baada ya kikao hicho kumalizika," alisisitiza Zungu.

Mwishoni mwa wiki kilisambaa kipeperushi chenye ujumbe wa kuhamasisha mgomo kufanyika kuanzia jana, kikieleza kwamba hakuna duka litakalofunguliwa eneo la Kariakoo na yeyote atakayeonekana amefungua atashughulikiwa.

Sehemu ya kipeperushi hicho kilisomeka:

"Wafanyabiashara wote wa Kariakoo mnatakiwa kufunga biashara zenu zote yakiwamo maduka na ofisi. Chochote unachokifanya kuanzia Jumatatu Juni 24 bila ukomo hadi pale changamoto zetu zote za kibiashara zitakapotatuliwa."

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya, Romana Mallya (DAR) na Paul Mabeja (DODOMA).**

# Mbowe asema mwakani ni mpambano CDM, CCM

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema Watanzania wanachopaswa kutambua na kukiweka akilini kuelekea Uchaguzi Mkuu mwakani ni kwamba, mpambano utakuwa ni wao na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aidha, amewataka askari wa Jeshi la Polisi, kuacha mpambano huo uchezwe kama mechi ya Simba na Yanga kwa kusimamia kiapo chao cha kulinda raia na mali zao, kwa kuwa mali za raia nyingine ni pamoja na kura zao.

Mbowe alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi wa Waso, Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro jijini Arusha.

"CCM hakitaki hoja ya Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi, hawataki kwa sababu wanajua wakienda kwenye uchaguzi ulio huru na wa haki, watawatandika asubuhi misa ya kwanza.

"Tumewaambia wenzetu tunataka Tume Huru ya Uchaguzi, tunataka Katiba Mpya ili uchaguzi wetu uwe huru na haki, hawataki.

"Nimeona askari polisi hapa, niwaambie ndugu zangu wa polisi, mateso wanayoyapata Watanzania wote ni pamoja na ninyi. Na mateso haya yanasababishwa na CCM. Acheni kuwa machawa wa CCM, acheni kuwasaidia CCM. Simamieni haki katika nchi yetu," alisema.

Aliwaeleza askari polisi kwamba, wamekula kiapo cha kulinda raia na mali zao, hivyo mali za raia ni pamoja na kura zao.

"Askari wetu simamieni kiapo chenu, msiwe mawakala wa kuisaidia CCM. Tuachieni hiyo ngoma tucheze nao kama Simba na Yanga," alisema Mbowe.

Alisema wananchi wa maeneo ya Loliondo, wamewaambia hawako tayari kuirejesha CCM katika uchaguzi mkuu ujao.

Katika mkutano uliofanyika Jumamosi, Mang'ola na Eyasi, Wilaya ya Karatu, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu, alihadharisha kwamba, Maofisa Watendaji wa Vijiji (VEO), watakaoengua wagombea wao katika mchakato huo, hawatabaki salama.

"Mimi ninasema mchana kweupe. Ofisa mtendaji wa kijiji atakayeengua mgombea wetu yeyote; hawa watendaji wanakaa wapi, si wanakaa na sisi mitaani huku, akiengua mgombea wetu mwambieni kabla hatujafika huko, ukiengua mgombea wetu hubaki.

"Achilia mbali kuwa Mwenyekiti wa Kijiji au Kitongoji, ninataka tushindwe kwenye kura tu. Tunataka wananchi watukatae kwenye kura tu, tusishindiwe mezani, tusishindwe kwa wagombea wetu kuenguliwa," alisema Lissu.

Alisema kwa sasa wana jukumu la kujipanga kwa mwaka ujao kurudisha heshima ya Karatu na Mang'ola, warudishe uchumi wake na rasilimali zake.

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi akataa kuongezewa muda u-Rais

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya mjadala kuhusu pendekezo la kuongezwa muda wa uongozi kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kutoka miaka mitano hadi saba, mwenyewe amepinga na kusema ataongoza kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Taarifa iliyotoka Ikulu jana na kusainiwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Charles Hilary, imesema kuwa Rais Mwinyi ataendelea kuheshimu utaratibu uliowekwa wa kuchaguliwa kila baada ya miaka mitano.

“Rais Dk. Mwinyi ni muumini wa kufuata Katiba na sheria za nchi, tunapenda kusisitiza kwamba maoni hayo kuhusu kuongezwa muda, sio ya rais wala sio ya Chama Cha Mapinduzi Zanzibar,” ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema maoni hayo pia yamekwenda mbali zaidi hata kutaka uchaguzi mkuu wa mwakani wa kumchagua rais wa Zanzibar usifanyike, jambo hilo halina tija wala faida kwa nchi na Chama Cha Mapinduzi chenye kufuata misingi ya demokrasia.

Taarifa hiyo, imewataka wananchi wenye mawazo tofauti na hayo wafunge mjadala huo.

Mjadala huo uliibuka baada ya Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Mohamed Said Dimwa, kusema Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati Maalum ya CCM, Zanzibar wamepitisha pendekezo la kuishauri kamati maalum kuridhia kuongeza muda wa Rais wa Zanzibar kuongoza nchi katika muhula wake kwanza kwa kipindi cha miaka saba badala ya mitano.

**CCM: HAKUNA MPANGO KUMWONGEZEA MUDA**

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, CPA Amos Makalla, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinaendeshwa kwa vikao na hakuna mpango wa kumwongezea muda wa kuongoza nchi, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Katika mahojiano maalum na Globaltv yaliyofanyika jana jijini Dar es Salaam, Makalla alipoulizwa kuhusu suala la Zanzibar, alisema juzi na jana alilisikia jambo hilo na kuona kwenye vyombo vya habari.

“Niseme mimi ni Katibu wa Uenezi CCM, mimi ndiye ninayesema mambo yote ya chama katika vikao, mimi ninaingia katika Sekterarieti, ninaingia Kamati Kuu, ninaingia Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

“Chama chetu kinaendeshwa na vikao kwa hiyo sijaona kikao chochote ambacho kitanifanya mimi nishindwe kuelewa uwapo wa jambo hilo.

“Niseme tu taarifa zinazosambaa hazipo katika utaratibu wa vikao vya chama chetu na nilivyosoma nimeelewa kwamba ni mawazo, lakini hata kile kikao cha Zanzibar ambayo ni Kamati Maalum Mwenyekiti wake anakuwa Makamu Mwenyekiti na Rais wa Zanzibar, nako halijafika kwa hiyo mawazo ni mawazo,” alisisitiza Makalla.

Hata hivyo, Makalla aliomba anukuliwe; “mimi kama msemaji wa chama, chama chetu kinaendeshwa kwa vikao na taarifa hiyo sina na mpango huo haupo. Aliwaomba Watanzania kuwa hilo jambo halipo na kwamba, Chama Cha Mapinduzi kinaheshimu utawala wa sheria.

“Tunajua kuna Katiba na ukisoma Katiba ya Zanzibar Ibara 28(2) (i) kinaeleza kwamba, Rais wa Zanziabr atakaa miaka mitano na baada ya hapo kutakuwa na uchaguzi vivyo hivyo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.”

Makalla alisema ili kuthibitisha hilo wametoka kujadili suala la bajeti na tayari serikali imewasilisha bajeti ikiwamo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani.

“Kwa hiyo haiwezekani kukawa na jambo hilo wakati suala hilo tayari lipo kwenye bajeti na kila chama kinajiandaa na harakati zake kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo niwatoe hofu Watanzania, mawazo yanaruhusiwa yamesemwa ni mawazo, lakini hayajapita katika vikao rasmi vya Chama Cha Mapinduzi,” alisisitiza.

Dk. Dimwa alisema uamuzi huo wa kumwongezea muda Rais Mwinyi wa kuongoza nchi unatokana na kuridhishwa na kasi yake ya kiutendaji katika kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa zaidi ya asilimia 100 ndani ya kipindi cha miaka mitatu na miezi kadhaa toka aingie madarakani.

Katika maelezo yake, Dk. Dimwa alisema kuwa CCM Zanzibar imeona serikali kuingiza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ni hasara na matumizi mabaya ya fedha za walipakodi kwa kuwa wananchi wanahitaji maendeleo endelevu na Rais Dk. Mwinyi anafaa kuongezewa muda, ili Zanzibar iwe nchi ya visiwa iliyoendelea kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Awali, akizungumzia kuhusu ajenda na hoja ambazo huibuka kuelekea Uchaguzi Mkuu, Makalla alisema siku zote lengo la chama cha siasa ni kushika dola na kamwe hakihubiri kwenda mbinguni.

“Dola inaanza na kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndio maana umetuona tumekuwa kwenye ziara ndefu ya mikoa 11 kuhamasisha viongozi wa ngazi zote kujiandaa na uchaguzi na mwakani, tukishinda vizuri tutashinda kwa kishindo,” alisema.

Makalla alisema ndani ya CCM wanajiona wako salama, wako imara na kauli yao ni umoja ni ushindi.

Alisema walipopita katika mikoa walichokiona ni uhai wa chama upo vizuri na wanaona watashinda kwa kishindo katika uchaguzi huo.

Tofauti na wenzao, alisema wameona uchaguzi wao wa ndani haujawaacha salama, kumekuwa na makundi, mgawanyiko wa viongozi mbalimbali wakati CCM uchaguzi ukiisha wanahakikisha hauleti makundi na wanapotoka nje wanakuwa wa moja.

***Imeandikwa na Rahma Suleiman (ZANZIBAR) na Romana Mallya (DAR)**


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI

TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Vikundi vya Wanawake na Vijana(Makundi maalumu) na Kozi ya lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 26/08/2024 – 21/09/2024 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |
| 2 | Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)** 30/09/2024 - 26/10/2024 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

**(a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:**

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na mada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha Wanawake na Vijana (washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**(b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:**

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ujenzi wa barabara za lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na mada shirikishi ambazo ni: Mada juu ya vifaa na Mitambo midogo midogo, Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na matengenezo ya barabara za lami.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya Lami kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki nne (4) ni Kiingereza; kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

**a) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana**

i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo kwa gharama ya ada kiasi cha Tsh. 700,000.

**b) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads)**

i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo kwa gharama ya ada kiasi cha Tsh. 1,000,000.

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**

**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# Mfanyakazi wa TANAPA na familia yake wazikwa

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

VILIO na simanzi jana vilitawala katika Kijiji cha Shigatini, Tarafa ya Ugweno, Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, baada ya mwili wa askari wa daraja la kwanza wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na wanawe watatu wa kike mili yao kuwasili nyumbani kwao Lomboni kwa maziko.

Askari huyo na wanawe, Mariam Zuberi (9), Salma Zuberi (7) na Bisma Zuberi (3), walipoteza maisha baada ya makazi yao kuteketea kwa moto wakiwa wamelala Juni 22, Olmatejoo jijini Arusha.

Miili yao iliwasili jana saa 6:00 mchana kwa magari maalum ya TANAPA na kuzikwa saa 10:00 jioni katika makaburi ya familia ya Msemo, yaliyoko kitongoji cha Lomboni.

Askari huyo wa uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, alirejea Arusha ilipokuwa familia yake kwa ajili ya kumpa hongera mkewe aliyekuwa amejifungua wiki moja iliyopita.

Watoto wake watatu walipoteza maisha papo hapo wakati moto ukiendelea kuteketeza nyumba yao na baba mzazi wa watoto hao, Zuberi alifariki dunia Juni 23, wakati akipatiwa matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Waombolezaji na ndugu wa marehemu, akiwamo Twahia Msuya, wameeleza kuwa vifo vya pamoja vya ndugu zao vimeacha pengo kubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, aliwaongoza mamia ya waombolezaji katika maziko ya familia hiyo.

Akizungumzia tukio hilo juzi, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani humo, Jeradi Nonkwe, alisema chanzo cha moto huo ni kompyuta mpakato (laptop) iliyokuwa imechomekwa kwenye soketi ya umeme kushika moto na kuunguza kochi.

Watu wengine saba walionusurika akiwamo mtoto mchanga wa siku nne, walikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount.

Majeruhi wanaoendelea kupatiwa matibabu ni mama wa watoto hao, Jasmine Khatibu (33), Mariam Mussa (60) ambaye ni mama mzazi wa Zuberi na Mwanaidi Aldina (50).

Wengine ni Mussa Msemo (34), AbdulKarim Ramadhan (9) na mfanyakazi wa ndani aliyefahamika kwa jina moja la Ester (20).



# NCAA yaonya upotoshaji wanaohama Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) imezitaka baadhi ya taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka ndani na nje ya nchi kuacha upotoshaji kuhusu wananchi wanaohama kwa hiyari ndani ya hifadhi hiyo.

Wananchi hao ni wale wanaojiandikisha kwenda Kijiji cha Msomera, NCAA imewataka wapotoshaji wa mchakato huo kutafuta ukweli kuhusu suala hilo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa tamasha la jamii ya Wamasai lililofanyika ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, Kaimu Meneja wa Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka hiyo, Hamis Dambaya, alisema baadhi ya taasisi zimekuwa zikiripoti kabila la Wamasai wanaoishi ndani ya hifadhi hiyo wanafukuzwa na kuondolewa kwa nguvu.

Alikanusha upotoshaji huo na kueleza kwamba, ndio maana hata tamasha hilo limefanyika ndani ya Kreta ya Ngorongoro na kuhudhuriwa na watu mbalimbali wakiwamo watumishi.

Alisema jamii ya Kimasai, Wahadzabe, Wamang'ati wanaoishi ndani ya hifadhi imekuwa na ushirikiano mkubwa na Mamlaka hiyo ndiyo maana uelimishaji wa wananchi kuhama kwa hiyari umekuwa ukifanyika bila upinzani wowote.

Dambaya alisema katika tamasha hilo mamlaka hiyo imeelimisha wananchi kuhusu huduma za kijamii ambazo serikali inazitoa katika Kijiji cha Msomera kulinganisha na maisha ya ndani ya hifadhi na baadhi yao kueleza kuwa wapo tayari kuwafuata wenzao.

'Kliniki ya Makonda'

# Rais Samia aagiza wenye magonjwa makubwa wapelekwe hospitali za serikali kutibiwa

**Na Beatrice Shayo,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amepiga simu wakati kambi maalumu ya madaktari bingwa ikiendelea jijini hapa na kuagiza watakaobainika kuwa na matatizo makubwa wapelekwe hospitali za serikali kwa matibabu zaidi.

Kambi hiyo ya siku saba iliyoanza jana iliyoandaliwa na Mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda, walijitokeza zaidi ya watu 5,000 wakiwamo wa mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Manyara.



Kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa wamelazimika kuweka utaratibu maalum wa kuhudumia baadhi, huku wengine wakitakiwa kurudi leo na wenye shida ya tezi dume na saratani wakibaki kupatiwa utaratibu wa matibabu.

Wakati huduma hizo zikiendelea, Rais Samia alimpigia simu Makonda mubashara akitaka kujua kinachoendelea.

"Nimekupigia ulinipa taarifa kuwa leo (jana) kutakuwa na kambi ya matibabu ndani ya mkoa huu, nilitaka kujua kama hiyo kambi imefanyika," aliuliza Rais Samia na kujibiwa imeanza na imepata madaktari na wauguzi zaidi ya 450 na dawa za kutosha huku, hospitali zote kubwa binafsi na za serikali zikiitikia wito.

"Lakini Mheshimiwa Rais Samia furaha tuliyokuwa nayo ni kuwapo kwa helikopta ya kumbeba mwananchi wa kawaida maskini na kumpeleka hospitali yoyote nchini Tanzania kwa ajili ya kupatiwa matibabu," alisema Makonda.

Hata hivyo, Rais Samia alipohoji kuhusu helikopta hiyo, Makonda alimweleza kwamba, wameipata kupitia wadau ambao wanahusika na utoaji wa huduma za afya mkoani humo.

"Wadau wa utalii wameunga mkono jambo hili ili kuhakikisha wananchi wanafikia huduma za afya kwa wakati baada ya kuelewa maelekezo yako na upendo uliokuwa nao kwa wananchi, hasa wanyonge na maskini ambao wanapambana na afya zao," alisema Makonda.

Rais Samia aliwashukuru madaktari waliojitolea pamoja na waliojitolea kuleta helikopta hiyo.

"Bila shaka hapo kutatakiwa mafuta kwa waliojitolea, maombi yangu kwa wananchi wajitokeze kufanya shughuli kama hiyo, ni jambo kubwa na lina gharama, hivyo wananchi wasipojitokeza gharama zitakuwa zimeenda bure.

"Niwaombe sana wananchi wa Mkoa wa Arusha, wajitokeze watumie fursa hiyo, na mimi nipo nyuma yao, Mkuu wa Mkoa kama kuna kitu chochote ambacho kinatakiwa kama kusaidia chakula ama mafuta, basi utuambie ili tuongeze nguvu kambi iende vizuri," alisema Rais Samia.

Pia, alisema ataangalia jambo la kufanya katika kambi hiyo kwa siku saba wanazowahudumia wananchi kuwekeza ili wananchi wapate matibabu.

Awali, Makonda alisema anatambua wapo wananchi ambao wanapata mateso katika afya na wengine kupoteza maisha, kwa sababu ya gharama kubwa za matibabu.

"Kuna wengine hawajui hata waende wapi, ili tuwe watumishi wazuri, lazima tuwatumikie hawa wananchi ukitoka hapa utapatiwa dawa, utapatiwa upasuaji bila kulipia tumekuja mbele yenu kuwatumikia ili mtukumbuke na sisi wakati wa uhitaji wetu watu wasimame kutupigania," alisema.

Makonda alisema kuna kipindi madereva wa bodaboda walimfuata na kumuomba mchango kwa ajili ya mwenzao aliyepata ajali na yupo hospitali anahitaji fedha ya kujitibu.

Alisema wanapokuwa na bima ya afya maana yake hawatahangaika kuchangisha watu katika kipindi ambacho wanahitaji matibabu.

Aliwaeleza kwamba, mgonjwa akayezidiwa katika kambi hiyo bila kujali ana fedha au la atapelekwa bure kwa helikopta hospitali za Mount Meru, KCMC au Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam na wenye matatizo ya macho kuna miwani ya bure 5,000.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema wamejiandaa kutoa vipimo na matibabu ya moyo na wale ambao watahitaji usaidizi wa karibu watawasafirisha bure kwenda Dar es Salaam kwa matibabu zaidi.

**WANANCHI**

Josephine Masawe, alisema licha ya kuwahi, ameshindwa kupata huduma kutokana na idadi ya watu kuwa kubwa, na kutatakiwa kurejea siku inayofuata.

Elisante Yacob, alipongeza kuwapo kwa kambi hiyo ya bure ambayo inawasaidia wasiojiweza kumudu gharama hospitalini.

Alisema alipatiwa namba 337 na tayari amemwona daktari na kupewa dawa kwa ajili ya tatizo lake kutokana na kupata ajali na mkono kuvunjika na kumsababishia maumivu makali.





KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wanawake wasikwamishwe kugombea uongozi

**BAADHI** ya wanawake hukatishwa tamaa kugombea nafasi za uongozi kisiasa kutokana na vikwazo wanavyokumbana navyo.

Wengine wanakosa ujasiri wa kuthubutu baada ya kuona wenzao wanavyopata misukosuko ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa kwenye majukwaa.

Hali hiyo inathibitishwa na baadhi ya viongozi wanawake waliowahi kushika nyadhifa za juu serikalini na kwenye taasisi mbalimbali, mikikimikiki waliyopambana nayo mpaka kufanikiwa kushika uongozi.

Miongoni mwa sababu zinazowadhoofisha wanawake wengi kujitokeza kuwania nafasi iwe kwenye siasa au taasisi ni kuombwa rushwa ya ngono.

Kuna wanawake wanaojitambua ambao wakishatajiwa suala la rushwa ya ngono, anaona isiwe tabu na kuamua kuendelea na mambo yake anayofanya kuliko kudhalilishwa.

Sehemu yoyote linapokuja suala la kupewa nafasi kwa upendeleo, ufanisi hukosekana kwasababu ya kukosekana kwa heshima.

Rushwa ya ngono ni kilio kikubwa sehemu za kazi na kwenye vyuo vya elimu ya juu.

Mtu hata kama ana haki ya kupandishiwa mshahara, au cheo anaweza kutafutiwa sababu ya kukwamishwa kwasababu tu hakutoa ushirikiano alipoombwa kutoa rushwa ya ngono.

Hii ni vita kubwa na inapaswa kukomeshwa na wanawake wenyewe kwa kujitambua na kutokubali kudhalilishwa kwa namna yoyote ile.

Kwenye nafasi za kisiasa, wanawake wengi hulalamika kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuitwa majina ya ajabu ajabu ili tu wakatishwe tamaa.

Kwa wanawake walio kwenye ndoa wanakuwa kwenye mtihani mkubwa baada ya wenza wao kusikia yanayofanyika kwenye mchakato wa kuwania nafasi hizo na kuamua kuwakataza ili kuepuka kashfa.

Suala hili linahitaji kukemewa na pia elimu ya kutosha kuanzia mijini na vijijini ili wanawake wengi waelimike na kujitokeza kuwania nafasi.

Vyama vya siasa, wanaharakati wa haki za binadamu mna kazi kubwa ya kutoa elimu kupiga vita jambo hilo.

Kwa kudhoofisha wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, kunaweza kukapoteza ari yao ya kuonyesha vipaji vyao vya uongozi.

Na katika maeneo mengi ya kazi imeshuhudiwa kuwa wanawake wanapopewa uongozi wanafanya vizuri na hata suala la rushwa ya ngono huwezi kulisikia.

Mapambano ya rushwa ya ngono ni lazima yawe makubwa ili kukomesha hali hiyo kabisa.

Aidha, wanawake wajitahidi kuhamasishana wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali wasibakie kuwa wapiga kura.

Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa, lakini bado hawajitokeza kwa hofu ya udhalilishaji.

"Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji, juhudi zifanyike wafikiwe. Rushwa ya ngono ni kikwazo, waume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," anasema aliyewahi kuwa waziri wa zamani Shamim Khan.

Mwanamke akitaka kugombea nafasi yoyote anapaswa kukataa rushwa ya ngono na akiwa na heshima yake hakuna atakayemfuata.

Pia ni muhimu wakajua kanuni na vyama vya siasa vifanye bidii kupeleka kanuni hizo hadi ngazi ya chini ndipo watapatikana wanawake wengi.

Kuna nafasi za viti maalum vya udiwani na ubunge, ambazo zimependekezwa na wadau wa siasa ziwe na ukomo wa miaka kumi ili kutoa nafasi kwa wanawake wengine kuziwania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Sabato Kasika

### Muungwana Lazima Nilonge

## Uje ufumbuzi waliorejeshwa shule kushindwa kusoma

**NI** miaka minne sasa wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ya kupata mimba wako shuleni kuendelea na masomo kama kawaida.

Tangu mwaka 2021 serikali imetangaza kuwaruhusu warudi shuleni kuendelea na masomo.

Baada ya tangazo hilo, wakuu wa vyuo vya maendeleo ya jamii walielekezwa kuwawekea mazingira ambayo yatawezesha wanafunzi hao kusoma bila changamoto.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa kwenye baadhi ya maeneo wanafunzi hao waliorejea shuleni wanakumbwa na vikwazo vingi ikiwamo huduma duni za lishe na uangalizi kwa watoto wao.

Hiyo ni pamoja na hali ngumu ya kiuchumi kukidhi mahitaji ya kujikimu yao pamoja na watoto wao na kusababisha wakate tamaa ya kuendelea na masomo kwa ajili ya kutimiza ndoto zao kielimu.

Baadhi ya wadau wa elimu wakiwa mkoani Mbeya hivi karibuni huku wakishirikiana na Shirika la Haki Elimu, walifanya tathmini ya mpango wa kuwarejesha shule wanafunzi hao shuleni na kubaini hayo.

Kama changamoto hizo zipo, ninadhani bado wazazi na walezi wana nafasi ya kusaidia kuzitatua, hasa kwa kuzingatia kwamba serikali imefanya sehemu yake kwa kuwaruhusu warudi shuleni.

Changamoto hizo, zinaweza kuwa ndani ya uwezo wa familia na wale waliowapa mabinti hao mimba, badala ya kulalamika huku watu hao wapo wanaendelea na maisha kama kawaida.

Lakini kama watu hao hawatoi huduma, hilo pia linaweza kuwa fundisho la kuwafanya mabinti kuwa makini na kuepuka kuingia katika vishawishi ambavyo matokeo yake ni kukatisha masomo.

Sasa kama serikali imetoa nafasi lakini zinaibuka changamoto za aina hiyo, ambazo ni wazi zinatakiwa kutatuliwa na familia za waathirika wa mimba hizo ili waweze kusoma bila kikwazo.

Taarifa iliowahi kutolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilionyesha kuwa hadi kufikia Januari, 2023 wanafunzi waliopata ujauzito na kurejea shuleni kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari ni 1,907.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa wizara hiyo, Omary Kipanga ni kwamba wanafunzi 562 kati ya hayo 1,907 wamerudi katika mfumo rasmi, huku waliorejea nje ya mfumo huo kupitia mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) wakiwa ni 1,345.

Wizara inasema inaendelea kukusanya taarifa za wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kukatiza masomo kwa sababu mbalimbali. Binafsi ninaamini inawezekana idadi ikaendelea kuongezeka.

Lakini jambo la msingi ni kwamba, wazazi na wale waliowapa mimba mabinti hao wakahusika kikamilifu kumaliza matatizo, kwani inawezekana wengi wakakwama kuendelea na masomo.

Kila upande ukiwajibika, ni wazi kile ambacho serikali imekusudia cha kutaja mabinti watimize ndoto zao katika elimu, kinaweza kutimia, lakini upande mwingine ukijiweka pembeni na kudhani hauhusiki, si sahihi.

Ikumbukwe kuwa mimba za utotoni ni pale mtoto wa kike wa kuanzia umri wa miaka 10 hadi 18 anapopata ujauzito na kujifungua. Mara nyingi kundi la umri huo huwa shuleni katika ngazi ya msingi au sekondari.

Mara nyingi sababu za mabinti wa umri huo kupata mimba katika umri mdogo ni ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi, changamoto za wazazi kutengana, umaskini, hivyo ni vyema wanaosababisha mimba hizo wahusike kikamilifu katika huduma.

Kwa miaka mingi, wanafunzi waliopata mimba, hawakuruhusiwa kurudi shuleni, lakini sasa serikali imeruhusu, ni vyema hatua hiyo imepewe uzito ili kuwapunguzia vikwazo wawapo masomoni.

**Lakini kama watu hao hawatoi huduma, hilo pia linaweza kuwa fundisho la kuwafanya mabinti kuwa makini na kuepuka kuingia katika vishawishi ambavyo matokeo yake ni kukatisha masomo.**

# Meli kubwa ya kontena 4,000 yatia nanga Dar

**N a Joseph Mwendapole**

BANDARI ya Dar es Salaam imeweka rekodi kwa kupokea meli kubwa ya mizigo yenye urefu wa mita 294.1 iliyobeba kontena 4,000.

Meli ya mwisho kupokewa ilikuwa na urefu wa mita 267 hatua inayotafsiriwa kama sehemu ya mafanikio ya uwekezaji uliofanywa katika bandari hiyo.

Meneja Mizigo Mchanganyiko wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus, alisema hayo baada ya meli hiyo kuwasili bandarini hapo na shehena hiyo.

Alisema meli hiyo ya (MSC ADU -V) imekuwa ya kwanza kubwa kuwasili katika bandari hiyo.

"Hii ni historia kwetu kwani hapo awali tulikuwa tunapokea meli zenye urefu wa mita 267, lakini sasa tuna uwezo wa kupokea meli zenye uwezo ukubwa wa mita 305 haya ni mafanikio makubwa kwetu kama Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA)," alisema Abed.

Alisema uwekezaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kupitia TPA katika Bandari ya Dar es Salaam umechangia kiasi kikubwa kuongezeka ufanisi wa kiutendaji.

Awali, bandari likuwa na kina cha wastani wa mita nane mpaka 12.7, lakini sasa kimeongezwa na kufikia mita 14.5 na kuwa na uwezo wa kupokea meli zenye urefu wa mita zaidi ya 305.

"Tunazipongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali ambayo imewekeza vya kutosha katika Bandari ya Dar es Salaam ikiwamo kuongeza kina na vitendea kazi katika bandari yetu na hivyo kutoa matokeo chanya ikiwamo kuanza kupokea meli kubwa," alisema.

Aidha, moja ya faida ya kubwa kupokea meli kubwa za mizigo ni kupungua kwa gharama za kusafirisha mizigo na kuleta unafuu kwa wafanyabiashara na wasafirishaji wa mizigo, na kuchochea ushindani wa bandari zilizopo ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Kumekuwa na ufanisi mkubwa ikiwamo kuhakikisha upakuaji wa mizigo unafanyika kwa haraka zaidi kwani ndani ya saa 24 tuna uwezo wa kupakua wastani wa kontena 800 hivyo tunatarajia ndani ya siku tano meli hii itakuwa imeshapakua na kuondoka katika bandari yetu," alisema Abed.

Alisema Bandari ya Dar es Salaam ni miongoni mwa sita ambazo TPA inazisimamia na kwa kuliona hilo mamlaka imeendelea kuboresha nyingine ili kutoa msaada kwa Bandari ya Dar es Salaam ambayo zaidi ya asilimia 95 ya mizigo inapita katika bandari hiyo.

"Tumeendelea kuboresha miundombinu ya bandari zetu ikiwamo pamoja na Bandari ya Mtwara na Tanga ambapo tayari tumeshanunua vifaa vya upakuaji mizigo kwani hapo awali Bandari ya Tanga, meli zilikuwa zinafungwa nje ya gati, lakini sasa hivi meli zinaingia kwenye gati," alisema.

"Uboreshaji huu wote ni juhudi za mamlaka kuhakikisha bandari hizo zinatoa msaada kwa Bandari ya Dar es Salaam," alisema Abed.

TPA imeingia mikataba ya kiuendeshaji katika baadhi ya gati zake kwa Bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi na kufanya bandari hiyo kuwa kinara kwa uingizaji na usafirishaji wa mizigo kwa nchi nyingi zikiwamo za Maziwa Makuu na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

# TCRA yaja na mkakati kuibua vinara kidijiti

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA harakati za kuhakikisha Tanzania inaandaa vinara wa kidijiti watakaokuwa na misingi imara ya kutatua changamoto na kuleta suluhisho za kuendesha shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo kidijiti, TCRA imekuja na mkakati imara wa kufikia malengo hayo.

Moja ya mikakati hiyo ni kuundwa na kuanzishwa kwa klabu za kidijiti kuanzia kwa wanafunzi wa ngazi ya awali hadi vyuo vikuu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, akielezea faida za klabu za kidijiti alisema ni nyenzo muhimu ya kuwakutanisha wanafunzi mbalimbali kujadili na kubadilishana uzoefu kwenye masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati (STEM) na TEHAMA.

Dk. Jabiri aliongeza kuwa vijana wanatakiwa watumie fursa hiyo ipasavyo kwa kuwa itasaidia kuipaisha nchi ya Tanzania kupitia uchumi wa kidijiti.

Baadhi ya wanufaika mbalimbali wa klabu hizo wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi kutoka Unguja ambao ni Ibtisam Khalfan Abdallah (Skuli ya Turkish Maarif), Sarinah Salmin Sharif (Skuli ya Laureate), Zuhra Said Salum (Skuli ya Salim Turky) na Balqis Salum Khamis (Skuli ya Bububu), waliobuni mfumo wa kununua umeme na kuweka ankara za umeme kwenye mita za LUKU moja kwa moja, walisema wanawahamasisha wanafunzi wenzao kutumia fursa hiyo ipasavyo.

Walisema itawawezesha kuja na mbinu mbalimbali za kuendesha nchi kidijiti na ni muhimu kufanya hivyo kwa kuwa uchumi wa sasa unaendeshwa kwa mapinduzi ya teknolojia.

Wanafunzi wengine wa shule za msingi kutoka Pemba ambao ni Hidaya Mohmed, Ahlam Ali (Michakaini A) Kauthar Mohmed (Al Khamis Camp) na Rayyan Masoud (Michakaini B), walisisitiza kuwa fursa hiyo kwao imekuwa muhimu na wanaahidi kuongeza vipaji vyao.

Walisema wameona matunda ya klabu za kidijiti ndani ya muda mfupi na baada ya kujiunga na klabu za kidijiti wameanza kupata matokeo chanya na mfano mzuri ni namna walivyofanikiwa kuja na suluhisho la kutoa elimu ya usalama mtandaoni.

Klabu za kidijiti hazikuishia tu shule za msingi, bali pia zilifika mpaka shule za sekondari, baadhi ya wanufaika wa klabu hizi kutoka shule ya sekondari Kijitonyama, Dar es Salaam ambao ni Tupokigwe Gwamaka, Keyline Mathias, Princess Wilfred, Ilham Suleiman, Rosemary Sanonga na Irene Basiga walielezea jinsi klabu ilivyowasaidia kubuni mradi unaohusisha michezo yenye manufaa kwa wasichana (Interactive ICT Career Exploration Game for girls).

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA MPANGO WA KUWAWEZESHA VIJANA KIUCHUMI KUMBUKUMBU NA: REQ-00000513**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP LTD) inaalika makampuni au taasisi zenye uzoefu na sifa nzuri kuonyesha nia yao ya kufanya Upembuzi yakinifu kuhusu Upatikanaji wa huduma za Maji kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Kampuni ya EACOP inajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**
Kampuni ya EACOP inapita na imetwaa ardhi katika takribani jamii 30 za makabila ya pembezoni yanayojitambulisha kama watu wa Asili katika mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma na Tabora. Kama sehemu ya ahadi yake kwa jamii hizi zilizorejelewa katika mikataba mbalimbali na kwa kuzingatia Viwango vya Fedha vya Kimataifa, EACOP sasa inatafuta taasisi zenye uzoefu na sifa nzuri kutoa huduma kwa jamii hizi maalum za makundi haya ya pembezoni wanaojitambulisha kama Watu wa Asili (maelezo yatatolewa wakati wa wito wa zabuni):

- **00000513 – 01:** Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi: shughuli zitajumuisha kuwajengea uwezo katika mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji; kurahisisha mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji; kusaidia kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi; kurahisisha upatikanaji wa CCROs;
- **00000513 – 02:** Kuimarisha Uwezeshaji wa Wanawake na Vijana kupitia kuunda vikundi na kukuza mazingira bora ya biashara kwa vijana na wanawake pamoja na kutambua fursa za kuunganisha vikundi vya vijana na wanawake na taasisi zinazotoa msaada wa ujasiriamali husika.
- **00000513 – 03:** Kuimarisha Jamii: Kuunda na kuimarisha Kamati za Maendeleo ya Jamii ya Kijiji na kutekeleza shughuli za kuwajengea uwezo katika ngazi ya jamii.

Katika kufanya kazi hii, EACOP inahitaji taasisi moja au zaidi (za kibinafsi au zisizo za kiserikali) zenye rekodi thabiti ya uzoefu katika kufanya kazi na jamii hizi kuhusu masuala haya.
Muombaji anaweza kuomba vipengele vyote tajwa au akaomba kipengele kimoja au viwili kulingana na uwezo wake.

**VIGEZO MUHIMU:**
Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, ujuzi kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana ikiwa ipo.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au ametuma maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP Database) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani (Compliance with Petroleum Local Content Regulation,2017)
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **14/07/2024.** Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA 00000513: KWA AJILI YA MPANGO WA KUWAWEZESHA VIJANA KIUCHUMI.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

# TAKUKURU yawaonya wenye ulemavu kutumika kutoa rushwa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewataka watu wenye ulemavu Mkoa wa Singida kutokubali kuwa mawakala wa wagombea kwa kushiriki kutoa rushwa wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu na uchaguzi wa mkuu wa 2025.

Ofisa wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Joseph John, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo kwa watu wenye ulemavu yenye lengo la kuwajengea uelewa wa masuala ya rushwa hasa katika kipindi cha uchaguzi.

Alisema wajibu wa watu wenye ulemavu kama raia wema wa Tanzania ni kutoa taarifa wanapobaini kuna vitendo vya rushwa na kutoshiriki kupokea na kutoa.

"Mwaka huu na mwakani tutakuwa na uchaguzi, na serikali imeshatoa kanuni za uchaguzi, sasa msikubali kuwa mawakala wa wagombea katika kutoa rushwa au jambo lolote ambalo limekatazwa kisheria," alisema.

Naye Ramadhani Mrisho alisema wenye ulemavu wanapata vikwazo vingi wakati uchaguzi, ikwamo wakati mwingine mifumo kutowatambua hali ambayo inasababisha wakose haki ya kupiga kura.

Alisema mafunzo yakiyotolewa na TAKUKURU sasa yatawapa uelewa na kujiamini ni namna gani wataweza kukabiliana na changamoto zinazowakabili wakati wa uchaguzi.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, amewataka wananchi kuacha kuwafuata wanasiasa wanaohamasisha wananchi wasijitokeza kupiga kura wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Msange, alisema kuna baadhi ya wanasiasa wanapita pita katika maeneo mbalimbali kuwataka wananchi kuacha kupiga kura katika chaguzi zijazo, wakati ni haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi.

Mlata alisema serikali itaendelea kudumisha amani, utulivu na Muungano wa Tanzania, ili wananchi waendelee kufanya shughuli mbalimbali kwa utulivu za kujiletea maendeleo na taifa kwa ujumla.

Alisema wapo baadhi ya wanasiasa wanasema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hauna faida yoyote, na kwamba wanasiasa hao sio wakuwasikiliza wala kufuata maneno yao kwa kuwa hawalitakii mema taifa.




Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Zainab Abdallah, akimkabidhi zawadi ya viungo vya chakula, Naibu Waziri wa Maji, Kundo Mathew, baada ya kuzungumza na madiwani wa halmashauri hiyo na kukagua miradi ya vituo vya maji katika eneo la Kilapula. Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Salim Sechambo (wa pili kushoto) na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Mhina (kulia). **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Miche 500 ya mikarafuu yapandwa Moro kuinua uchumi

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

BODI ya Maji Bonde la Wami Ruvu (WRBWB) imepanda miche 500 ya mikarafuu katika maeneo mbalimbali ya wananchi yaliyo jirani na vyanzo vya maji mkoani Morogoro ili kulinda mazingira huku ikiinua uchumi wa wananchi.

Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Mhandisi Elibariki Mmasi alisema, katika mwaka ujao wa fedha wanatarajia kupanda miche ya miti aina ya mikarafuu 20,000, miparachichi 5,000 kutoka mkoani Njombe na migomba kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Mmasi alisema Mkoa wa Morogoro una vyanzo vya maji vingi huku zaidi vikiwa katika maeneo ya Milima Uluguru na wakazi wa maeneo hayo wanatamani kutumia maeneo yao kwa ajili ya kilimo ili kukuza uchumi wao.

Alisema katika kulinda mazingira kwa mujibu wa sheria wanahakikisha mwananchi anapata faida katika miche ya miti inayopandwa na wameanzisha upandaji wa miche ya miti ya mazao kulingana na eneo na uhitaji wa wananchi ili kutunza vyanzo vya maji.

Aidha, alisema hali ya maji katika maeneo ya bonde ni stahimilivu kwa shughuli zote za kiuchumi ikiwamo kilimo na shughuli zingine na wanaendelea kufuatilia kama kuna changamoto yoyote na kuwajulisha wadau mapema ili kuepusha hasara za uwekezaji zinazoweza kujitokeza.

Aliishukuru serikali na wadau wa maji kwa tija kubwa ya uwekezaji wa ujenzi wa mabwawa hasa Bwawa la Kidunda ambalo ana uhakika litasaidia kuondoa adha wanayoipata wakazi wa Dar es Salaam ya kukumbwa na mafuriko yanayotokana na mtiririko mkubwa wa maji yanayoelekea baharini hasa wakati wa masika.

Naye Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Morogoro Mhandisi Sospeter Lutonja, alisema wanatarajia kuyafikia maeneo yote ya vijiji kwa asilimia 95 ifikapo mwezi Desemba, mwaka 2025.

Mhandisi Lutonja alisema RUWASA kwa sasa inahudumia zaidi ya vijiji 669 mkoani Morogoro na hali ya upatikanaji wa maji imefikia asilimia 65.57 na kwamba kwa kushirikiana na bonde la maji wanaendelea kutafuta vyanzo vya maji ili kuvifikia vijiji ambavyo bado hawajavifikiwa.

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Musa Ally Musa, aliwataka wadau wa maji na mazingira kwa ujumla kuzingatia upandaji miti hasa ya mazao ya biashara ili kuinua uchumi wa wananchi wa eneo husika.

"Tukipanda miti tukumbuke miti ya mazao ambayo inadumu na kuleta manufaa kwa wananchi hasa mikarafuu, ikipandwa, maana yake ni fedha, ikipandwa 40 tu ambayo inaingia katika heka moja ni milioni 19 mpaka 13, hizo tayari zinatosha kumtoa mtu au familia katika janga la umaskini," alisema.

Alisema upandaji wa miti una faidi kwa kuleta vivuli pia na kwa mazao ya biashara kama vile michaichai, migomba na miparachichi ambayo inaweza kuwaondoa wananchi katika umaskini.

## TANESCO yaendelea maboresho mita za LUKU

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WATEJA wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Kanda ya Kusini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, wametakiwa kuendelea na maboresho ya mfumo wa Lipa Umeme Kadili Unavyotumia (LUKU) hadi Novemba 24, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano kwa Umma wa TANESCO, Irene Gowele, alisema maboresho hayo yanalenga kuendana na viwango vya mifumo ya LUKU ya kimataifa na kuongeza ufanisi zaidi pamoja na usalama wa mita za LUKU nchini.

Gowele alisema kazi hiyo inaanza rasmi Juni 24, mwaka huu katika mikoa ya Mtwara Lindi, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Rukwa, Njombe na Songwe na amewashauri wateja wa shirika hilo kujitokeza kuhakikisha inafanikiwa kama ilivyo kusudiwa.

Alifafanua kuwa mteja atakaponunua umeme kwa mara ya kwanza kuanzia tarehe tajwa atapokea tarakimu kwenye makundi matatu kila moja likiwa na tarakimu 20.

Alisema kundi la kwanza na la pili la tarakimu litakuwa kwa ajili ya maboresho na kundi la tatu litakuwa la tarakimu la umeme utakaokuwa umenunuliwa na mteja, ambaye ataingiza tarakimu la kila kundi kwa mfuatano unao someka kwenye risiti ya malipo au ujumbe mfupi wa simu (SMS) na kila atakapo ingiza kundi moja mteja atapaswa kubonyeza alama ya kukubali ya reli # au mshale wa kukubali na hapo atakuwa amefanikiwa kuboresha mita yake na kupokea kiwango cha umeme aliounuua.

Alisema uboreshaji huo utafanyika mara moja kwa mteja na ataendelea kupata kundi moja la tarakimu 20 kila anapofanya ununuzi wa umeme.

Alisema baada ya mikoa hiyo uboreshaji huo utaendelea kwa mikoa mingine nchini kwa awamu kadiri TANESCO itakavyotangaza kwa umma na mwisho ni Novemba 24, mwaka huu.



## Usajili vyama vya ushirika mfumo wa kisasa wasuasua

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

OFISA Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', William Mbogoro amesema hadi sasa ni vyama vya ushirika 108 katika Mkoa wa Manyara, vilivyojiandikisha katika mfumo wa kisasa 'Move' .

Alisema kanzidata ya serikali inaonyesha kuwa vyama 35 bado havijajiandikisha, huku wanachama 9,603 wakiwa tayari wako kwenye mfumo huo na wanachama 4,025 wako nje ya mfumo.

Alitoa taarifa hiyo jana wakati akitoa taarifa ya ushirika ya mkoa huo kwenye Jukwaa la Maendeleo ya Vyama vya Ushirika mkoani Manyara.

Kwa mujibu wa Mbogoro, mkoa huo una vyama vya ushirika 143; ambapo vyama hai ni 99, na vyama sinzia 44.

Aidha, alisema ili wanaushirika waendelee kunufaika na mazao yao ni vizuri wauze kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeishatoa waraka kwa halmashauri zote kuusimamia ili wakulima wasiibiwe.

"Mwaka jana tuliuza zaidi ya kilogramu milioni moja za mazao mwaka huu tunaomba tushiriki kwenye mfumo huu tusikubali kunyonywa na walanguzi, sasa hivi tutafanya kupitia TMX na siyo mabox," alisema Mbogoro.

Ofisa huyo alisema Ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani humo, inaendelea kusimamia vipaumbele saba vya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, ambavyo ni uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidigitali, kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika, biashara ya mazao na kufanya uwekezaji.

Alitaja vipaumbele vingine ni kuboresha sera, sheria na usimamizi wa vyama vya ushirika, kuhamasisha ushirika katika sekta mbalimbali ya makundi maalumu, kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika katika uwekezaji na ushirikiano na wadau mbalimbali.

Hata hivyo, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalum Cheliga, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, alisema ustawi wa vyama vya ushirika unategemeana na wamiliki wenyewe wa vyama vya ushirika.

Cheliga alitumia fursa hiyo kuwaelekeza wakulima kujipanga vizuri kuutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kuuza mazao ya mbaazi, ufuta, dengu, alizeti na mazao mengine ya biashara.

Awali, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Yuda Sulley, aliwaomba wanaushirika kupitia vyama vyao kuwa wanatenga bajeti kwa ajili ya kushiriki katika Jukwaa la Maendeleo ya Vyama vya Ushirika mkoani Manyara.

# Wadau sekta ufugaji nyuki duniani kukutana Tanzania

**Na Godfrey Mushi,**
NGORONGORO

RAIS wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani (Apimondia), Dk. Jeff Petiz, ametangaza neema kwa wafugaji wa nyuki nchini, huku akiitaka Tanzania kujiandaa kupokea ugeni wa watu 6,000 kutoka mataifa mbalimbali wanaokuja kujadili masuala ya ufugaji nyuki na masoko.

Amesema Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa wadau wa nyuki utakaofanyika mwaka 2027.

Dk. Petiz, alieleza hayo alipotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwa mapumziko, alisema wadau hao wa sekta ya nyuki watajadili na watatoka na azimio kuhusu changamoto za uzalishaji, masoko, mnyororo wa thamani na bei ya zao hilo duniani.

Katika ziara hiyo, Dk. Petiz, aliambatana na Rais wa Kamisheni hiyo Kanda ya Afrika, David Mukomana.

Akiwa Ngorongoro alipongeza Menejimenti ya NCAA, kwa jitihada za utunzaji wa hifadhi hiyo ambayo imeendelea kuvutia maelfu ya watalii.

Dk. Petiz alisema: "Sijawahi kuona sehemu nzuri kama Kreta ya Ngorongoro maishani mwangu. Nimeona wanyama wakubwa ambao ni faru, tembo, simba, chui, nyati na wengineo ndani ya muda mfupi wakiwa katika eneo moja wakiwa kwenye mazingira yao ya asili".

Aliongeza: "Hakika nimepata uzoefu usiosahaulika maishani mwangu, kuona eneo la pekee lililotunzwa na kuwepo wanyama wa kila aina na kushuhudia idadi kubwa ya wageni ni jambo la kupendeza na hakika eneo hilo kila mmoja anapaswa kulitembelea katika uhai wa maisha yake."

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, aliyembatana na Dk. Petiz, aliipongeza Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhifadhi eneo hilo mashuhuri duniani katika nyanja za utalii, uhifadhi, utamaduni na kupambana na mimea vamizi.




Wanaushirika mkoani Manyara wakiwa kwenye maandamano ya amani mwishoni mwa wiki iliyopita katika barabara kuu ya Babati/Arusha wakati wakielekea kufanya jukwaa la maendeleo ya vyama vya ushirika, mkoani humo, ili kujadili namna ya kuboresha ushirika kwa maendeleo ya wakulima. **PICHA: JALIWASON JASSON**

## Halmashauri yaagizwa kulipa madeni ya bil.2.3/-

**Na Hamida Kamchalla,**
HANDENI

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, ameiagiza Halmashauri ya Handeni Vijijini kulipa madeni ya Sh. bilioni 2.306 inayodaiwa na watumishi na wazabuni mbalimbali.

Deni hilo ndilo linalochangia kuongezeka kwa hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Dk. Buriani alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha baraza maalum la madiwani, lililoketi kupokea taarifa za CAG kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

"Kwa mfano madeni ya watumishi, Handeni ndiyo halmashauri pekee kushinda halmashauri zote yenye madeni mengi ya watumishi na wazabuni.

"Lakini pia hata ule utayari wa kulipa hauonekani na fedha mnayotenga kulipa ni ndogo. Fedha mnayotenga ni Sh. milioni 24, hii tunaona kama ni takrima. Haipendezi hawa watu wanakwenda mpaka kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kudai madeni yao," alisema.

Mbali na deni hilo la watumishi na wazabuni, Mkuu huyo wa Mkoa, aliielekeza halmashauri hiyo kulipa deni la Sh. milioni 17 kabla ya Juni 30 mwaka huu, inalodaiwa na watumishi wastaafu.

"Hili ni deni la kufuta kabisa, tuhakikishe kabla ya kufika Juni 30, deni la watumishi wastaafu liwe limefutwa. Kuna mambo mengine ambayo ni lazima tuyasimamie na kuyatekeleza wenyewe," alisisitiza.

Awali, akitoa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkoa wa Tanga, Hamu Mwakasola, alisema katika mapendekezo 41, sawa na asilimia 71 yametekelezwa, mengine 17 bado hayajatekelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Handeni Vijijini, Steven Saitoti, alisema kuwa watahakikisha yale yote ambayo yaliibuliwa kwenye taarifa ya hoja za CAG, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, wanakwenda kuyatekeleza kwa vitendo.





# Walia kutolipwa fidia mradi wa bomba la mafuta Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati na kuhakikisha wanafidiwa maeneo yao yaliyochukuliwa ili kupisha Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti, Eliainaswa Elibariki, mkazi wa Zongomela na Christina Kasumbai, walisema baadhi ya wananchi wameshalipwa fidia isipokuwa kuna baadhi hawajalipwa hadi sasa.

Alisema wao walipewa maeneo na serikali kwa lengo la kuyaendeleza katika shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo, lakini mpaka sasa wamekosa fidia na badala yake wamepisha mradi ili wasije kuonekana ni kikwazo cha utekelezaji wake.

“Eneo lililopita bomba la mafuta ghafi tulipewa na Manispaa ya Kahama, wakati huo ikiwa Halmashauri ya Mji mwaka 2016 ili tuyaendeleze na tuliyaendeleza kwa kuweka misingi na kujenga nyumba, mwaka 2023 tuligundua tunapitiwa na mradi huo, lakini hakuna fidia yoyote tuliyopata,” alisema Elibariki.

Hivyo, aliiomba serikali kuingilia kati na kuangalia namna ya kuwapatia fidia kama walivyofanya katika maeneo mengine walipopita mradi huo.

Naye Christina Kasumbai, alisema baada ya kugundua eneo lake limepitiwa na mradi huo aliwatafuta wanaohusika kujua taratibu za kufuata ili apate kulipwa fidia, lakini hakuweza kupata majibu ya kuridhisha.

Hivyo, aliamua kwenda halmashauri na alipofika alipewa majibu kwamba eneo hilo tayari limeshalipwa fidia.

Akijibu hoja hiyo kwa njia ya simu, Ofisa Mawasiliano wa EACOP, Abbas Ibrahim, alisema eneo linalolalamikiwa linamilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, tayari waliishailipa halmashauri hiyo fidia kama waguswa wa mradi na siyo wao (wananchi) waliopewa eneo hilo kuliendeleza kama wanavyodai.

Katibu Tawala wa Wilaya Kahama, Hamad Mbega, alisema baada ya kupokea malalamiko hayo alilazimika kufuatilia ili kujua uhalali wa madai na kugundua kwamba eneo hilo tayari limelipwa fidia.

Alisema wameamua kukaa na Ofisi ya Mkurugenzi kujua namna gani wanaweza kutatua sambamba na kuwapatia maeneo mengine wakazi hao.



Wakulima wa pamba katika kijiji cha Buzilayombo Wilaya ya Chato mkoani Geita, wakipima pamba wakati wa masoko mkoani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# RC atoa siku 30 wanakijiji kumaliza mgogoro wa mpaka

**Na Rose Jacob,** BUTIAMA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Evans Mtambi, ametoa muda wa mwezi mmoja kwa wakazi wa vijiji vya Bumangi na Kinyariri wilayani Butiama, kukubaliana wapi panapaswa kuwekwa mipaka ya vijiji hivyo.

Alitoa agizo hilo baada ya kufanya kikao cha pamoja na wakazi wa vijiji hivyo, kufuatia uwepo wa mgogoro wa ardhi unaohusu mipaka kati ya vijiji hivyo, mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka 25.

“Kaeni mkubaliane kama mpaka unatakiwa kufuata ramani ya mwaka 1973 au hii ya mwaka 1996 ifanyiwe maboresho, natoa agizo hili baada ya kubaini kuwa kuna shida hapa na lazima shida hii ifike mwisho, tunataka kuzungumza maendeleo na siyo migogoro,” alisema Mtambi.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu mipaka ya vijiji, pande zote husika zinapaswa zikae pamoja na kuainisha mipaka kwa pamoja, jambo ambalo halikufuatwa wakati wa uchoraji wa ramani na uwekaji wa mipaka mwaka 1996.

“Watu wa Bumangi wamesema wao walishiriki, lakini wa Kinyariri wamesema hawakushirikishwa, ingawa mchakato wa mwaka 1973 ulishirikisha pande zote, nia ya serikali ni kutaka kuona jamii yenye amani na maendeleo yatapatikana katika jamii isiyokuwa na migogoro, hivyo serikali ya mkoa haipo tayari kuwa na jamii iliyojaa migogoro,” alisema Mtambi.

Wakizungumzia mgogoro huo, wakazi hao walidai chanzo cha mgogoro ni uwepo wa mwekezaji katika Kijiji cha Bumangi, Mauza Nyakirang'anyi aliyewekeza kijijini hapo tangu mwaka 1992 ambaye wamedai alimega maeneo ya Kijiji cha Kinyariri bila kufuata utaratibu.

Naye mkazi wa Bumangi, John Iranga, alisema mipaka ya vijiji hivyo ipo kwenye milima iliyopo katika eneo hilo, huku wakazi wa Kijiji cha Kinyariri wakidai mpaka upo kwenye mto ulio jirani.

Aidha, Meneja wa shamba la kilimo na ufugaji la Mahuza Nyakirang'anyi, Emmanuel Buzanza, alisema mwekezaji huyo amefuata taratibu zote za uwekezaji.

Alisema: “Eneo letu lina ukubwa wa ekari 123 na tulifuata taratibu zote, ingawa wapo wananchi ambao wanaingia katika eneo letu sisi na siyo kwamba sisi tumemega maeneo ya kijiji cha Nyakiriri.”

# Mkandarasi uwanja wa ndege akalia kuti kavu

**Na Rose Jacob,** MUSOMA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Evans Mtambi, amesema hajaridhishwa na kasi ya mkandarasi anayetekeleza mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma.

Hivyo, ameuagiza Wakala wa Barabara Nchini (Tanroads) Mkoa wa Mara kumsimamia mkandarasi huyo.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo ambapo alisema visingizio vilivyotolewa juu ya kuchelewa kwa mradi havikubaliki, hasa ikizingatiwa umuhimu wa mradi huo kwa maendeleo ya mkoa na watu wake.

“Kwa mkandarasi aliyejiandaa vizuri hawezi kushindwa kufanyakazi kisa anadai Sh. bilioni tatu wakati tayari amelipwa zaidi ya Sh. bilioni 10, Tanroads nawaagiza simamieni mradi huu kwa ukaribu na muwe wakali, nami kuanzia sasa nitakuwa nafanya ziara hapa mara kwa mara,” alisema.

Alisema kutokuwapo kwa uwanja wa ndege mkoani hapa kwa namna moja ama nyingine kumekuwa kukirudisha nyuma jitihada za wakazi wa mkoa huo kujiletea maendeleo, hivyo uwanja huo unapaswa kukamilika kwa wakati ili utoe huduma zilizokusudiwa.

Kuhusu fidia za watu 50 wanaotakiwa kupisha maeneo kwa ajili ya mradi huo, alisema tayari suala hilo linashughulikiwa na kwamba muda wowote watu hao watalipwa.

“Hili suala linajulikana wizarani na hata Waziri Mkuu alipokuja huku nilimweleza na alisema analijua na linafanyiwa kazi, niwahakikishie wananchi kuwa lazima watalipwa na malipo yamechelewa kidogo kwasababu ya uharibifu wa miundombinu uliotokana na mvua zilizonyesha nchini, hivyo serikali ililekeza nguvu nyingi kurejesha mawasiliano kwanza,” alisema.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja wa Tanroads Mkoa wa Mara, Vedastus Maribe alisema mradi huo ulioanza Aprili, 2021 ulitarajiwa kukamilika Desemba 2023 lakini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwepo kuchelewa kwa malipo pamoja na mitambo ya mkandarasi kuwa mibovu haukuweza kukamilika.

Alisema: “Hadi sasa mradi huu unaotekelezwa na mkandarasi Beijing China Engine Group kutoka China kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 35 umefika asilimia 57 na mkandarasi amelipwa zaidi ya Sh. bilioni 10 huku akidai zaidi ya Sh. bilioni tatu”.

Alisema wakazi 50 walio jirani na mradi huo wanadai Sh. bilioni 3.9 za fidia ili waweze kupisha katika maeneo yao.

Alisema uwanja huo unatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami ambapo pamoja na mambo mengine ujenzi huo unahusisha ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege, njia ya maungio, ujenzi wa maegesho ya ndege, jengo la zimamoto na gari la zimamoto pamoja na uzio.



Ukurasa 12

**Hifadhi ya sokwe yaweza kuwa kisima dawa asilia**



Ukurasa 13

Vinara, mbumbumbu kielimu barani Afrika

Nipashe

# TESA

Jumanne Juni 25, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

**Kufanya juhudi hizi kutarejesha uoto asilia na kutunza mazingira**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

NGONO MTANDAO

# Matangazo, picha zashamiri kwa kasi

• Janga mmomonyoko wa maadili kwa vijana

MAENDELEO ya sayansi na teknolojia yanachangia kukuza uchumi na kuibua mambo mengi ya kisasa yakiwamo yanayopotosha, kama kuchochea ngono mitandaoni.

Leo maisha yamebadilika huduma kuanzia tiba, elimu, biashara, mitindo ya mavazi, magari na uwekezaji wa aina zote hufanikishwa na mtandao.

Zama hizi za kujifunza au kupata elimu na ujuzi mbalimbali lakini pia kuuza na kununua mitandao, zinawaibua wale wanaofanyabiashara za ngono pia, wakisaka na kupeana miadi na wale wanaotaka kushiriki matendo hayo, iwe nje au ndani ya nchi.

Mambo hayo ya kufanya biashara rasmi za ngono kwenye nyumba au madanguro, yalishamiri zaidi Ulaya na Amerika na kwa Tanzania si jambo linalokubalika tena ni jinai kuwa na madanguro na kuuza ngono hadharani.

Wenye biashara hizo nao wako mitandaoni wakitangaza popote duniani kusaka wateja au kuwaalika kutembelea madanguro yao.

Kuiga mbinu hizo na kutumia mitandao kumechangia kuibua wadau kutoka Tanzania nao wakisaka wateja, wanunuzi, wauzaji na hata maajenti, wanaofanyakazi hiyo mitandaoni . Inadaiwa kuwa kwa baadhi ya mabinti wanaojiuza na maajenti wanaosaka wateja wao wasichana ni chanzo cha kipato.

Miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Zanzibar ni maeneo ambayo unaweza kupata biashara ya aina hiyo ikiendelea watu wakitumia simu za kujinadi na kujitangaza pamoja na kuweka gharama zao na maeneo ya wanakopatikana.

Mitaani bado kuna wanaouza miili yao mfano jijini Dar es Salaam Ubungo Riverside, Buguruni Kimboka, Sinza, Afrika Sana, Posta na Kariakoo ni sehemu zinazoongoza kwa watu wanaofanyabiashara hizo nyakati za usiku.

Lakini biashara ya ngono mtandaoni inavyoelekea inakua siku baada ya siku kutokana na maendeleo ya teknolojia ambayo huenda ikiwaondoa kina dada hao mitaani wakabaki kufikia wateja kwa njia ya Facebook, WhatsApp, Instagram, TikTok, Telegram, Snapchat na X au tweeter na Youtube.

Utafiti unaofanywa na Nipashe unabainisha kuwa wengi wananunua na kuuza ngono mtandaoni tena bila kificho.

Imebainika kuwa wanawake kuanzia miaka 20 hadi miaka 35 ndiyo wanafanya biashara ya aina hiyo ambayo wanadai ina faida kwao, wakati wa mahojiano na gazeti hili.

"Wafanyabiashara wengi wa ngono wanajitangaza kupitia mitandao, mfano wanaweza kukutana na watu mashuhuri duniani na kupata fedha zaidi . Kwa mfano kwa kutumia..." anasema mmoja wa wahusika.

Wanataja baadhi ya mitandao wanayoitumia na kwamba siyo ile inayoruhusiwa nchini kwa mfano VPN.

"Biashara hiyo inafanywa kwa njia ya siri sana ambayo watu hutumia simu janja kuingia katika tovuti wanazofanya mambo hayo kwa kutumia mtandao binafsi kuepusha kukamatwa," anaongeza.

Wapo wanaopeleka picha na vivutio ngono mbalimbali ili kuvuta wateja sehemu mbalimbali ili wazichague na kuwasiliana, anaeleza zaidi.



Maumbile ni kivutio kinachoweza kutumiwa na mabinti kuvuta wateja mitandaoni. **PICHA: MTANDAO**

**INAENDELEA UK.12**

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Hifadhi ya sokwe yaweza kuwa kisima dawa asilia

KATIKA jitihada za kutafuta dawa kutibu magonjwa mbalimbali, watafiti wanawachunguza sokwemtu kuona jinsi wanavyokabiliana na maradhi kwa kula jamii za mimea kwenye misitu wanapoishi.

Kwa mujibu wa BBC, sokwemtu wanakula mimea inayotuliza maumivu, kuponya magonjwa na kuzuia bakteria au vimelea kujipenyeza ndani ya miili ya wanyama hao.

Watafiti hao wanafanyakazi katika misitu ya Uganda kuangalia baadhi ya wanyama hao ambao walikuwa wamejeruhiwa au wagonjwa ili kujua wanajitibu kwa mimea au kitu kingine.

Wakati mnyama aliyejeruhiwa alipotafuta kitu au mmea, jani, gome au tunda maalum kutoka msituni na kula, watafiti walikusanya sampuli za mmea huo na wakafanya vipimo zaidi kwenye maabara.

Mimea mingi iliyopimwa iligundulika kuwa na nguvu ya kupambana na bakteria. Wanasayansi, ambao walichapisha matokeo yao katika jarida la PLOS One, wanadhana kuwa sokwe wanaweza kufanikisha kutafuta dawa mpya za mitishamba.

"Hatuwezi kupima kila kitu katika misitu hii kwa lengo la kujua sifa zake za dawa, mtafiti mkuu Dk. Elodie Freymann, kutoka Chuo Kikuu cha Oxford, anasema."



Sokwe wakiwa hifadhini. **PICHA: MTANDAO**

"Kwa hivyo kwa nini tusifanyie vipimo mimea ambayo tuna habari kuwa jamii hii ndiyo sokwe wanayoitafuta?" Anahoji.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Dk. Freymann, ametumia miezi kadhaa kufuata na kutazama kwa makini jamii mbili za sokwe-mwitu katika Hifadhi ya Msitu Mkuu wa Budongo nchini Uganda, inaongeza BBC.

Pamoja na kutafuta dalili za maumivu, mnyama akichechemea au kuushika mwili wake kwa njia isiyo ya kawaida yeye na wenzake walikusanyika sampuli za kinyesi na mkojo ili kuangalia aina ya ugonjwa na maambukizi.

Wanaongeza umakini zaidi wakati sokwe aliyejeruhiwa au mgonjwa alipotafuta kitu ambacho kwa kawaida wanyama hao hawakili kwa kawaida.

Kitu hicho ni kama vile magome ya mti au ngozi ya matunda mbalimbali.

"Tulikuwa tunatafuta dalili hizi za kitabia kwamba mimea inaweza kuwa dawa," Dk. Freymann anaelezea.

Anaongeza kuwa walimfuatilia sokwe mmoja dume aliyekuwa na mkono uliojeruhiwa vibaya.

"Hakuwa akitumia mikono kutembea, alikuwa akichechemea," anakumbusha.

Wakati wengine walikuwa wameketi kula, sokwe aliyejeruhiwa alijikongoja akitafuta mmea uitwao fen, alikuwa sokwe pekee aliyetafuta na kula 'fen' hizo.

Watafiti walikusanya na kuchambua mmea huo unaoitwa Christella parasitica, ambao uliibuka kuwa na sifa za kuzuia mlipuko wa maambukizi ya bakteria.

Kwa jumla, watafiti walikusanya sampuli 17 kutoka aina 13 tofauti za mimea na kuzipeleka kufanyiwa majaribio na Dk. Fabien Schultz, wa Chuo Kikuu cha Neubrandenburg cha Sayansi nchini Ujerumani, inasema BBC.

Hiyo ilifichua kuwa karibu asilimia 90 ya mimea hiyo ilizuia ukuaji wa bakteria, na theluthi moja ilikuwa na sifa za asili za kuzuia ongezeko la maambukizi, ikimaanisha kuwa zinaweza kupunguza maumivu na kuongeza uponyaji.

Sokwe wote waliojeruhiwa na wagonjwa walioripotiwa katika utafiti huu walipona, Dk. Freymann, anasema na kuongeza kuwa anafurahisha.

"Aliyekula feni alikuwa akitumia mkono wake kwa ufanisi tena ndani ya siku chache zilizofuata baada ya tiba," anaeleza katika mahojiano na BBC.

"Bila shaka, hatuwezi kwa asilimia 100 kuthibitisha kwamba kesi yoyote kati ya hizi ni matokeo ya moja kwa moja ya kula miti dawa hiyo," anasema.

Anaongeza: "Lakini ni muhimu kutilia mkazo ujuzi wa kitiba unaoweza kupatikana kwa kuchunguza viumbe vingine porini na kusisitiza uhitaji wa haraka wa kuhifadhi misitu ambayo ni kama 'maduka ya dawa' kwa ajili ya vizazi vijavyo."

Kwa Tanzania sokwe mtu wanapatikana Hifadhi ya Gombe na Mahale mkoani Kigoma.

# Ngono Mtandao; matangazo, picha zashamiri kwa kasi

**INATOKA UK.11**

Mitandao ya kijamii imekuwa na jukumu katika ukuaji wakazi ya ngono mtandaoni, kwa mujibu wa maelezo yake.

Wahusika wanafafanua kuwa kutokana na mmomonyoko wa maadili mitandao hiyo huruhusu wafanyabiashara ya ngono kufikia wateja popote walipo.

Akizungumzia tatizo hilo la biashara hiyo mitandaoni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Mtandao wa Jeshi la Polisi, Joshua Ishekazoba, anasema kuwa serikali inapinga vikali biashara hiyo.

"Kwanza kuweka picha za utupu kwenye mitandao ya kijamii ni kinyume cha sheria. Hivyo kwa wale wanaojihusisha na biashara ya ngono mtandaoni wajue kuwa wanakwenda kinyume na sheria za nchi."

Kwa mujibu wa sheria ya usalama wa mtandao ya mwaka 2017 adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano jela au faini ya Shilingi milioni 20 au vyote kwa pamoja.

Anaitaka jamii kutoa taarifa za matendo hayo wanapowajua wahusika ili washtakiwe.

Mwanasaikolojia Rajab Ali, mhitimu wa elimu ya saikolojia, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anazungumzia mienendo hiyo akisema mara nyingi wanaofanya biashara hiyo wanafanyiwa ukatili wakikutana na hao wateja wa mitandaoni.

"Wanaofanya biashara hiyo mara nyingi hupata misukosuko na msongo wa mawazo japo hawawezi kukuonyesha ila ni wathirika wakubwa sana wa afya ya akili na wakati mwingine baadhi hufanya maamuzi mabaya na magumu," anasema Ali.

Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wanasema katika jamii yenye maadili watu wamekuwa na mtazamo kuwa biashara hiyo haifai na kwamba inawadhalilisha wanawake na vijana wanaojipandisha kwenye majuu ya biashara ya ngono.

Mwanafunzi wa sekondari Mariam Omary, anasema kuwa wanawake wanaofanyabiashara hiyo hawajithamini na kuwahimiza kusaka njia mbadala ya kupata riziki.

ANaonya kuwa kuishi biashara hiyo kunaweza kusabaisha magonjwa ya aina mbalimbali na athari za kiafya na kiakili.

"Inawapasa wabadilishe mtazamo ili kuacha hiyo biashara maana jamii yetu haiwachukulii vizuri na hawakubaliki. Ni kuvunja maadili ya taifa na heshima yetu," anaesema Mariam.

Vivyo hivyo Zakaria Kato-to, mwanajamii anayetumia mitandao kwa shughuli mbalimbali, anasema kuwa serikali inapaswa kuweka mkazo na kukataza mambo ili kujenga jamii iliyo bora kwa vizazi vyote.

Licha ya wanaohusika kukubaliana na kuwepo mambo hayo wajue kuwa kuna hatari na changamoto zinazotokana na kazi hiyo. Kwa Tanzania waojihusisha na biashara za ngono wengi wanakabiliwa na ubaguzi, unyanyapaa, chuki na hata kuchukiwa na baadhi ya watu mitaani.

Takwimu za Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), zinaonyesha kuwa vijana wengi wenye umri wa miaka 16 hadi 24 wameambukizwa VVU na UKIMWI, kwa hiyo ni vyema kujilinda na kujihami ikiwamo kuacha ngono za mitandaoni.

**Imeandaliwa na Neema Kassim, Paulo Peter, Flora Francis, Edna Mbwilo & Twaiba Swalehe**

# Vinara, mbumbumbu kielimu barani Afrika

## • Angola, Zambia chali idadi ya wajinga kubwa

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

ELIMU ni kila kitu, chanzo cha maendeleo tena ni kiungo muhimu katika kukua na kujenga uchumi endelevu, ndiyo maana nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania kila mara zinawekeza zaidi kuongeza ubora kwenye sekta hiyo.


Norway kwa sasa ndiyo inayoshika nambari moja duniani kwa kuwa na elimu bora kwa mujibu wa Kielezo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) cha Umoja wa Mataifa.

Marekani ni taifa kubwa lakini kwenye elimu linatajwa kuwa na elimu inayopatikana kwa gharama kubwa mno, lakini siyo kwamba ni bora zaidi.

Mwaka 2023 ripoti ya mtandao wa Bscholarly.com, unainukuu ripoti ya jukwaa la Elimu Duniani, inayochambua hali ya elimu kwenye nchi 140 na kati ya hizo mataifa 34 ya Afrika yanahusishwa.

Lengo ni kubainisha wapi kuna mfumo bora wa elimu unaozingatia kukuza ujuzi na stadi bora za kitaaluma pia kupika wahitimu mahiri na weledi.

Visiwa vya Shelisheli, ndilo taifa lenye elimu bora zaidi barani Afrika, vikiorodheshwa kuwa ni nchi pekee ya Kiafrika inayochuana na mataifa yaliyoendelea.



Miundombinu bora na walimu mahiri ni moja ya kigezo cha taifa kufikia elimu bora. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Kwa mfano, mwaka 2023 Shelisheli iliorodheshwa kuwa ya 43 kwa ubora wa elimu duniani ikizipita Ukraine, Hungary, Urusi na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Aidha, inaorodheshwa kuwa ya 28 duniani kwa kufundisha fikra tunduizi (critical thinking) na ya 34 kwa kuwa na ubora na umahiri kwenye wahitimu wanaozalishwa vyuoni.

Shelisheli ni nchi ya kwanza barani Afrika kukamilisha lengo la Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) la kutoa elimu kwa wote kikamilifu.

Taifa la pili kwa elimu bora Afrika ni Tunisia. Inashika nafasi ya pili. Elimu ya nchi hiyo ni ya lazima na inapatikana kwa wananchi wote kuanzia umri wa kwenda shule kuanzia madarasa ya awali hadi mtoto anapomaliza sekondari. Serikali inatumia asilimia 20 ya bajeti yake ya kitaifa katika sekta hiyo muhimu ya elimu.

Aidha, elimu bora inapatikana Mauritius, ikishika nafasi ya tatu, yenye elimu ya lazima kwa wananchi wake hadi mtoto afikishe umri wa miaka 16 ambapo lazima awe amemaliza shule ya sekondari.

Afrika Kusini inafuata ni ya nne kwa mfumo wa elimu bora ambao umepitia maendeleo na uwekezaji. Makadirio ya matumizi ya asilimia 18 ya bajeti ya nchi hiyo kuboresha kiwango na kuifanya iwe na ushindani wa kimataifa, ndiyo mwanzo wa kuwa na elimu bora.

Algeria ni taifa bora kielimu Afrika pia, inayoorodheshwa kuwa ya 88 kwa elimu bora katika mfumo wa elimu wa kimataifa na nchi 65 bora za Kiafrika katika umri wa kuishi shuleni.

Mbali na hilo, ni nchi ya tano kwa ubora barani Afrika, ikiwa na kiwango cha kusoma na kuandika cha asilimia 75 na alama 57.4 za wastani wa uelewa wa watu kwenye masuala ya elimu.

Algeria inaendesha mfumo wa elimu bila malipo kwa raia wake hadi wanapokuwa na umri wa hadi miaka 16.

Kusini mwa Afrika au ukanda wa SADC kuna Botswana ni ya sita kwa Afrika. Imeorodheshwa ya 92 kwa ubora katika mfumo wa elimu duniani, tena ni bora barani Afrika kwa kuzingatia umri wa kukaa shuleni.

Katika mafunzo ya ualimu duniani pia ina viwango vya juu ikiwa na kiwango cha kusoma na kuandika cha asilimia 88 kwa raia wake.

Kenya ni ya saba, ndilo taifa linalotisha kwa elimu makini Afrika Mashariki pia, imeorodheshwa kuwa ya 95 kwa ubora katika mfumo wa elimu duniani na ina asilimia 78.7 ya kiwango cha watu wanaojua kusoma, kuhesabu na kuandika.

Inashika nafasi ya 21 duniani katika kutafuta wafanyakazi wenye ujuzi wa kufundisha na kimataifa inapewa pointi 55.4 kwa juhudi za kuinua na kuendeleza elimu.

Elimu ni ya lazima kwa Wakenya kuanzia miaka sita hadi 17 na hutumia asilimia 17.58 ya bajeti yake katika sekta hiyo.

Cape Verde imeorodheshwa kuwa ya nane kwa elimu bora barani Afrika. Serikali yake inatoa elimu bila malipo kwa raia ambao wametimiza miaka 12 na ni lazima kwa watoto wenye umri wa miaka sita hadi 12 kusoma.

Misri ni taifa linaloshika nafasi ya 99 kwa ubora wa elimu duniani, ikiwa na asilimia 71 ya watu wanaojua kusoma na kuandika na pointi 52.8. Kwa mujibu wa UNESCO, Misri ni nchi ya 70 kwa ubora duniani katika masuala ya ujuzi wa kidijitali na inatoa elimu ya lazima na bila malipo kuanzia umri wa miaka sita hadi 15. Kwa Afrika inashika nafasi ya tisa.

Namibia imeorodheshwa kuwa ni ya 10 barani Afrika kwa kuwa na elimu bora. Pia ina asilimia 88.2 katika masuala ya kufikiri na kufundisha kwa kina duniani. Namibia ni ya 82 na 43 katika kutoa mafunzo bora duniani kote.

**MBUMBUMBU MKIANI**

Nchi inayoburuza mkia kwa elimu duni nambo moja ni Niger, ikiwa na watu milioni 21 lakini ina asilimia 28.7 ni mbumbumbu. Hawajui kusoma, kuhesabu wala kuandika.

> Elimu ni ya lazima kwa Wakenya kuanzia miaka sita hadi 17 na hutumia asilimia 17.58 ya bajeti yake katika sekta hiyo.

Inafuatiwa na Burkina Faso, kiwango cha mbumbumbu ni asilimia 27.7. Tatu ni Mali, nyingine ni Jamhuri ya Afrika ya Kati (Central African Republic) ina elimu duni mno na kiwango cha utoro ni cha juu ni ya pili kwa kuwa juu zaidi duniani.

Ethiopia haiko salama ni ya 5 kwa kuwa na kiwango cha chini zaidi cha Afrika na duniani. Ikifuatiwa na jirani yake Eritrea ni ya sita, kadhalika Gunea ni ya saba ikiwa na kiwango cha wengi wasiojua kusoma na kuandika wala kuhesabu, Zambia ya nane ikifuatiwa na Gambia na Angola inatisha ikishika nafasi ya 10 kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika, wala kuhesabu ni wengi pia.

Nchi hiyo ina viwango vya chini vya kusoma na kuandika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambayo inakadiriwa kuwa 33. Zaidi ya asilimia 50 ya watu hawajui kusoma na kuandika.

Katika Jamhuri ya Chad, zaidi ya asilimia 53 ya watoto wenye umri wa miaka 5-14 wanatumikishwa kwa watoto, na katika umri wa miaka 7-14 asilimia 30 ya watoto wanaenda shule, zaidi ya hayo, wanafanya kazi pamoja kama ajira ya watoto pia.

***Chanzo: Mitandao Edugist, Business Today***

ELIMU

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

# Kufanya juhudi hizi kutarejesha uoto asilia na kutunza mazingira

TANZANIA Bara ina miaka 63 ya uhuru na idadi ya watu, mifugo na wanyamapori inaongezeka kila mwaka. Huku eneo la ardhi likibaki lilelile.

Aidha, wakati mwingine kupungua, uzoefu ukionyesha kuwa chanzo kikubwa cha kupungua ardhi inayotegemewa kwa ufugaji na kilimo ni mmomonyoko wa udongo.

Kingine ni kumeguka ardhi kutokana na kasi kubwa ya maji ya mvua kwenye eneo lililoachwa wazi kupitia shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Kulingana na takwimu za sasa Juni 14, 2024 zinazotolewa na Umoja wa Mataifa kwa mfumo wa kidijitali "Worldometer", kiwango cha kutoweka misitu kidunia, kimefikia hekta milioni 2.4.

Kadhalika, kiwango cha kupotea ubora wa udongo (land loss) kutokana na sababu mbalimbali za kibinadamu ni hekta 3.2 milioni UN inasema.

Tanzania Bara, inakabiliwa na changamoto za kutoweka misitu asilia kwa kiwango cha hekta 372,000 kwa mwaka lakini pia tishio la kupoteza udongo au ardhi inayofaa kwa kilimo kutokana na mmomonyoko wa udongo au kumeguka ardhi sehemu mbalimbali. Hali hii hutokea kwenye miteremko mikali ambako kanuni za kilimo-hifadhi zimekuwa zinapuuzwa.

Wakati wa Uhuru 1961, hali ya vijito, mito kwenye mikoa yote ilikuwa nzuri. Kingo zake tangu mto ulipoanzia hadi mwisho unapoingia baharini, ziwani au bwawani zilifunikwa na uotoasili ambayo ni misitu, mimea pamoja na nyasi.

Kadhalika, vina vyake vilikuwa chini kulingana na ikolojia ya mahali, mathalani Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam, miaka ya 1970 maji yalikuwa yanatiririka yakiwa safi bila taka ngumu, uchafu wa kemikali au kusheheni udongo, mchanga na matope kama ilivyo sasa.

Nyakati hizi kina ni kifupi pembeni kuna vilima vya mchanga kandokando ya kingo za mto huo vinavyochotwa na katapila kuusafisha hasa eneo la Jangwani.

Miaka ya 1950 hadi 1980 mvua zilikuwa zinanyesha kwa wakati na nyingi kujaza mito na ilikuwa marachache kutokea madhara hatarishi kama ilivyo sasa.

Mfano miaka ya 1960 ilikuwa vigumu kuona kilele cha Mlima-Kilimanjaro kutokana na mawingu mazito juu yake. Kilikuwa kimesheheni theluji wakati misitu ikishikamana kuuzunguka mlima wote, leo theluji inatoweka kwa kasi huenda mlima ukabaki bila kufunikwa.




Katapila likisafisha takangumu na mchanga kupunguza mafuriko Jangwani yanayosababishwa na Mto Msimbazi. **PICHA: NIPASHE**

> Matokeo yake udongo mzuri husafirishwa kwa kasi kubwa ya maji inaponyesha mvua kubwa na kuikuta ardhi iko tupu bila kufunikwa na uotoasilia.

Pia Milima ya Uluguru ilikuwa inafunikwa na mawingu mazito hadi asubuhi. Vilevile, kulikuwapo na vijito vinavyotiririsha maji mwaka mzima. Kwa miaka hiyo haikushuhudiwa moto kwenye misitu asili kama ilivyokuwa kwa miongo mitatu iliyopita.

Kwa ujumla miaka hiyo, Tanzania Bara ilikuwa kijani zaidi maana nchi nzima ilifunikwa na uotoasili ikiwamo misitu mikubwa, mbuga zilizosheheni aina mbalimbali za mimea na nyasi pamoja na ardhioevu ya kutosha kuhifadhi maji ya mvua kwa muda mrefu.

Wakati huo, mito ilikuwa na maji ya kutosheleza karibu majira yote hata wakati wa kiangazi hayakukosekana.

Hali kama hiyo imebaki historia kutokana na shughuli nyingi za kibinadamu zisizokuwa endelevu hadi uotoasili kutoweka kwa kasi kubwa kusababisha kushamiri mimomonyoko ya udongo, mchanga na matope mpaka kumeguka ardhi.

Matokeo yake udongo mzuri husafirishwa kwa kasi kubwa ya maji inaponyesha mvua kubwa na kuikuta ardhi iko tupu bila kufunikwa na uotoasilia.

Matokeo yake mito husafirisha udongo, kemikali, mchanga na matope pamoja na takangumu hadi baharini, kwenye maziwa na katika mabwawa hivyo, kupunguza vina vyake kwa kiasi kikubwa.

Kinachoshuhudiwa leo ni matokeo hasi maana kwa zaidi ya miaka 60 ya uhuru, yamekuwa yakijitokeza taratibu lakini sasa kimefikia kiwango hatarishi.

Mvua zikinyesha mito inafurika maji haraka kiasi cha kuvuka kingo za mito na kusambaa haraka na kusababisha mafuriko yasiyotarajiwa. Vilevile, ardhi ya kufaa kilimo imekuwa ikipungua hivyo, taifa kukabiliana na athari za maeneo kadhaa kugeuka jangwa.

### NINI KIFANYIKE?

Mosi, nashukuru kwa hatua iliyochuliwa na viongozi wa kitaifa kukemea uharibifu wa mazingira na kuwataka wananchi kuchukua hatua kulinda mazingira kwa kupanda miti kwa wingi pia kuitunza misitu iliyokaribu nao.

Hili ni jambo jema la kupongezwa maana ni 'utashi wa kisiasa' kama ilivyojitokeza 2014. Watanzania wasilegeze kamba bali juhudi zipate msukumo kiasi kwamba miti ikioteshwa inatunzwa, inakua na kuonekana katika uhalisia wake.

Iwe ni ya matunda, mbao, nguzo, ya kivuli, yenye sifa za dawa, kupata kuni au mkaa, kuhifadhi maji, udongo na mazingira.

Aidha, juhudi zifanyike ili sheria na kanuni zilizopo zitekelezwe kuanzia serikali za vijiji, za mitaa hadi serikali kuu na taasisi zishirikiane na sekta binafsi kulinda mazingira.

Kwa mfano iwe kwenye shule za msingi, sekondari na hata vyuo vya kati na juu, iwapo sheria na kanuni hazitoshelezi, kwa kutokuwa na nguvu au kutotekelezeka ipasavyo, marekebisho yafanyike haraka.

Kadhalika vijito na mito, vyanzo vyake vilindwe (hasa misitu lindimaji) na maeneo mengine muhimu kama ardhioevu. Pia, kuhakikisha uotoasili unarejea kwenye ukanda wa mita 30/60 kutoka kingo za vijito na mito pande zote mbili.

Hali hiyo iwe tangu mto unapoanzia hadi mwisho wake mfano, kuanzia Mto Ruaha Mkuu na vijito vinavyoingiza maji uhifadhi wa kingo urejee.

Mto Rufiji na mingineyo yote inayoingiza maji baharini ilindwe ipasavyo. Kilimo cha aina yoyote kifanyike nje ya ukanda wa mita 60 kutoka ukingo wa mto kwa mito mikubwa na vijito mito midogo mita 30 ili kuondoa athari za mito kujaa udongo, mchanga na takangumu.

Bila kufanya hivyo, tutajikuta baada ya miaka kadhaa Bwawa la Mwalimu Nyerere litaonekana lina maji kumbe kina cha kuhifadhi maji kimepungua kutokana na kujaa udongo au mchanga.

Hali hiyo, ikiendelea kutokea taifa litapata hasara kubwa kwa kukosa umeme wa uhakika, sababu maji kupungua haraka.

Uhifadhi imara unatakiwa kwa mabwawa ya Mtera, Kidatu, Kihansi, Nyumba ya Mungu, na kwenye Mto Kagera Rusumo ili kulinda uhai wa mabwawa hayo.

Nyumba, mitaani na sehemu za kazi, usafi wa mazingira utamalaki na kila mhusika awajibike ipasavyo.

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa watakaochaguliwa kuwajibika ipasavyo. Wasiwe ni wa kuona mambo yanaharibika bila kuchukua hatua stahiki.

Watendaji kata wachakalike na magari ya kusomba takangumu yaonekane yakifanya kazi ipasavyo siyo tu katikati ya majiji, manispaa na miji bali hata sehemu zilizo nje ya hapo.

Jingine wataalamu wa kisekta wafanye utafiti wa kina kujua mpaka sasa mabwawa yameathiriwa kwa kiasi gani kutokana na kujaa udongo au mchanga na takataka nyingine, hatimaye waishauri serikali hatua za kuchukua kurejesha uhai wa mabwawa hayo.

Msisitizo wangu ni kuzisimamia sheria na kanuni zinazohusika kutunza misitu na mazingira na vyombo vinavyohusika visilaze damu wakati wa kulisaidia taifa na Watanzania ni sasa.





## Kanisa lawaonya vijana kutumika katika uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la Pentecostal Evangelistic Fellowship of Africa (PEFA) limewataka vijana nchini wasitumike kama daraja la wagombea watakaojitokeza kuwania nafasi za uchaguzi kwa kushawishiwa kupokea rushwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa vijana wa kanisa hilo, Mchungaji Samson Raphael, alipokuwa akizungumza na vijana kwenye kongamano la vijana lililoambatana na maombi katika Kanisa la Pefa Sayuni City Ntyuka Dodoma.

Mchungaji Raphael aliwataka vijana kutokubali kuwa madaraja ya kupitia wagombea hao kwa kupokea rushwa, ili waweze kuchaguliwa kwa njia zisizo halali zinazoweza kuvuruga amani na hata kuwapata viongozi wabovu wenye ubinafsi na wasiokuwa na maendeleo ya nchi.

Alisema kitendo cha kuwachagua viongozi hao kwa njia za rushwa ni dhambi na hata kwenye vitabu vitakatifu vimekemea utoaji rushwa.

Pia, aliwataka vijana nchini kuwa tayari kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kudumu pamoja na kuhakikisha wanapiga kura.

"Mwaka huu kuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji hapa nchini, niwaombe vijana kote nchini kwanza wajiepushe na vitendo vya kupokea rushwa, kujihusisha na uvurugaji wa amani na pia wale watakaokuwa na sifa na vigezo wajitokeze kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi," alisema.

Naye Askofu wa Jimbo la Dodoma PEFA, Jackson Taxgai, aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidii ili kuiletea nchi hii maendeleo ya kiuchumi badala ya kuinyoshea kidole serikali kwa kukosa kazi za kuajiriwa.

Alisema kuwa Tanzania kuna rasilimali nyingi za kujipatia kipato ikiwamo kujiajiri, hivyo ni wakati wao kwa vijana kutumia fursa hizo zilizopo kwenye uwekezaji uliopo kupitia sekta mbalimbali.

Alisema: "Hakuna sababu ya kukaa vijiweni na kwenye makundi ambayo hayana tija kwa ajili ya kujipatia kipato, badala yake wawe mabalozi wa kuhamasisha wenzao kuisaidia serikali na kanisa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kiroho".

# NEMC yapata mwarobaini wa matumizi ya zebaki

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linatarajia kutengeneza vifaa rahisi vya kuchenjulia dhahabu kama maeneo ya mfano ya teknolojia mbadala ya kuchenjua miongoni mwa wachimbaji wadogo nchini.

Vifaa hivyo vinavyotumia teknolojia rafiki kwa mazingira na afya za binadamu vinatarajia kutambulishwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo (EHPMP) unaotekelezwa na NEMC kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) kwa lengo la kupunguza matumizi na athari za zebaki kwa binadamu na mazingira.

Akizungumza wakati wa mafunzo maalumu ya uwajibikaji wa wachimbaji katika utunzaji wa mazingira migodini kwa wajumbe wa Shirikisho la Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA) kwenye maonesho ya wiki ya madini jijini Dodoma, Meneja wa EHPMP, Dk. Befrina Igulu alisema hatua hiyo inatarajia kuleta mapinduzi katika sekta ya uchimbaji wa dhahabu miongoni mwa wachimbaji wadogo.

Alisema hatua hiyo inakuja kutokana na utafiti kuonyesha kuwa wachimbaji wengi wadogo katika migodi ya dhahabu hapa nchini wapo katika hatari kubwa ya kupatwa na matatizo mbalimbali ya kiafya kutokana na matumizi yasiyo rafiki ya zebaki.

Alisema matatizo hayo ya kiafya ambayo tayari yameshaanza kuwapata baadhi ya wachimbaji ni pamoja na uharibifu wa figo, mfumo wa fahamu, kupoteza kumbukumbu, msongo wa mawazo, upofu, upungufu wa nguvu za kiume, kuharibika kwa mimba na watoto kuzaliwa na utindio wa ubongo.

Alisema kulingana na taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), zebaki ni miongoni mwa vyanzo 10 vinavyohatarisha afya ya jamii duniani.

Ili kudhibiti hali hiyo, alisema serikali kupitia NEMC na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali wanatekeleza mradi huo wa EHPMP kwa lengo la kuendesha jitihada kadhaa za kukabiliana na hali hiyo.

Alieleza kuwa mradi huo unaofadhiliwa na WB unalenga kusaidia kupunguza madhara ya zebaki kwa binadamu na mazingira nchini.

Dk. Igulu alisema rekodi zilizopo zinaonyesha kuwa Tanzania kila mwaka inaagiza na kutumia kati ya tani 18 na 21 za zebaki.

Aliitaja mikoa inayoongoza kwa matumizi ya kemikali hiyo kuwa ni Geita, Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Katavi, Lindi, Songwe na Mwanza.

Alisema lengo ni kuhakikisha sekta hiyo inaondokana kabisa na matumizi ya zebaki ifikapo mwaka 2030, hatua inayoendana na utekelezaji wa matakwa ya mkataba wa Minamata katika kupunguza au kuondoa kabisa matumizi ya zebaki lakini pia matakwa ya mpango kazi wa taifa.

Kama sehemu ya kutambulisha teknolojia hizo, alisema mpango ni kuanzisha vituo kadhaa vya kuonyesha na kutoa mafunzo kwa wachimbaji jinsi ya kuendesha (kutumia) teknolojia hiyo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi, akizungumza na wapigakura wake walipotembelea bungeni Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Uhamiaji watakiwa kujitathmini kila wakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, amewataka watumishi wa Jeshi la Uhamiaji kujifanyia tathmini kila wakati ili kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Alitoa rai hiyo jana mkoani Dodoma wakati akizungumza na watumishi wa jeshi hilo, kwenye kikao kazi baada ya kufanya ziara katika makao makuu ya Jeshi la Uhamiaji kwa ajili ya kufahamiana na watumishi.

Alisema viongozi wa jeshi hilo ambao wameaminiwa na Rais Samia Suluhu Hassan wanapaswa kujitathmini kila wakati wanapotekeleza majukumu yao ili kusimamia majukumu yao kwa weledi.

"Inabidi tuendelee kujitathmini kila siku katika utendaji wetu wa kazi ili kutekeleza majukumu yetu kwa weledi na ufanisi mkubwa," alisema Gugu.

Aidha, aliwataka watumishi hao kuwa wamoja kuishi kwa upendo ili kuweza kutekeleza maagizo ya serikali.

"Mheshimiwa Rais anataka mabadiliko na mambo mazuri kitaifa lakini hata humu ndani kwenu lazima muwe na upendo ili kuweza kufikia malengo," alisema.

Pia alisema jukumu la ulinzi wa geti la wageni kuingia nchini lipo chini ya watumishi wa Jeshi la Uhamiaji, hivyo watumishi hao wanawajibu wa kuhakikisha wanakuwa tayari kila wakati kuteleza majukumu yao.

"Kama una mambo yako kichwani yanayokusumbua jaribu kuyaacha nyumbani ili utekeleze majukumu yako ikiwa ni pamoja na kupokea wageni kwa ukarimu ili kufanya taasisi hii ifike pale tunapopataka," alisema.

Aliongeza kuwa kama kila mmoja ataelewa majukumu yake watafika pale ambapo Rais Samia Suluhu Hassan anapataka.

Kadhalika, aliwataka watumishi hao kwenda kuteleza bajeti iliyotengwa na serikali kwa mujibu wa sheria.

Gugu alisema: "Nimekuja wakati muafaka bajeti tayari imeshapita, hivyo basi nendeni mkaitekeleze kwa mujibu wa sheria hatutaki nyinyi kuichafua wizara kama mnajenga au mnanunua kitu basi iwe kwa mujibu wa sheria".



# Uwanja wa ndege wajengwa kwenye Hifadhi ya Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limezindua uwanja mpya wa ndege uliojengwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ambao utasaidia kuboresha shughuli za utalii na uhifadhi ndani ya hifadhi hiyo.

Uwanja huo wenye urefu wa km. 1.5 na eneo la maegesho ya ndege umejengwa na shirika lisilokuwa la kiserikali linalojihusisha na shughuli za uhifadhi la Six Rivers Afrika katika Kijiji cha Ikoga.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa uwanja huo, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwel Ole Meing'ataki alisema uwanja huo pia utasaidia kwenye shughuli za utafiti kwenye hifadhi hiyo.

Alisema uwanja huo utasaidia kufungua fursa za utalii katika Bonde la Usangu kwa maelezo kuwa tangu eneo hilo lilipoingizwa na kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha shughuli za utalii zilikuwa hazifanyiki vizuri kama ilivyo kwenye kanda zingine za hifadhi hiyo.

Alisema moja ya sababu ambazo zimekuwa zikikwamisha utalii katika eneo hilo hasa katika Bonde la Ihefu ni kukosekana kwa miundombinu bora ya usafiri na kwamba baada ya ujenzi wa uwanja huo watalii watafika kirahisi na kujionea vivutio.

"Uwanja huu ni matokeo ya ushirikiano ambao tumeingia na shirika hili, tumeshirikiana sana kwenye ujenzi wa huu uwanja, tulitoa eneo hili na kushirikiana na mamlaka mbalimbali za serikali zinazohusika na viwanja vya ndege," alisema Ole Meing'ataki.

Alisema vifaa vyote vilivyotumika kwenye ujenzi wa uwanja huo ni vya TANAPA na kwamba walivihamisha kutoka katika makao makuu ya shirika hilo yaliyoko Masembe ndani ya hifadhi hiyo.

Mwenyekiti wa Shirika la Six Rivers Afrika, Glenm Tuner alisema shirika hilo liliamua kushirikiana na Tanzania kwenye shughuli za uhifadhi kutokana na kuwa moja ya mataifa ambayo yanahifadhi vizuri maliasili.

Alisema asilimia 35 ya maliasili za Tanzania zimehifadhiwa vizuri na kwamba zikiunganishwa na zile za kwenye vyanzo vya maji inafika mpaka asilimia 40 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa taifa bora zaidi kwenye uhifadhi.

Alisema hakuna taifa lingine duniani ambalo limehifadhi rasilimali kama Tanzania na kwamba uhifadhi huo uliwafanya wajitolee kujenga uwanja huo pamoja na kushiriki kwenye shughuli zingine za uhifadhi.

"Lakini mbali na huu uwanja pia tunajenga chuo cha utalii katika eneo hili ili kuchochea zaidi uelewa wa wananchi kuhusu shughuli za uhifadhi na utalii," alisema Tuner.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alisema mbali na uwanja huo kuwahudumia watalii pia utawasaidia wananchi wa maeneo ya jirani kwa shughuli mbalimbali ikiwamo kuchochea shughuli za uzalishaji mali.

Hivyo, alishauri uwanja huo kuwekewa uzio ili kuepusha wanyama pori kuingia kwenye eneo la njia ya ndege akidai kuwa kuna uwezekano wakadhurika ama kusababisha ajali ya ndege.

Pia, aliushukuru uongozi wa shirika hilo kwa kuamua kushirikiana na Tanzania kwenye shughuli za uhifadhi, akidai kuwa ushirikiano huo utasaidia kuimarisha ulinzi wa rasilimali za taifa zilizoko kwenye hifadhi hiyo.

Alisema ndege zitakazokuwa zinaegeshwa kwenye eneo hilo zitasaidia pia kuboresha doria kwenye hifadhi hiyo ambayo imekuwa ikivamiwa na mifugo mara kwa mara.



Dereva wa bajaj iliyosheheni mizigo akiishusha katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mamalishe 100 kupewa mtaji wa kukuza biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMA lishe zaidi ya 100 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kunufaika na msaada wa mtaji ili waboreshe huduma zao na kukuza biashara.

Mtaji huo unatarajiwa kutolewa na Mjumbe wa Halmashauri ya Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela.

Mwaselela aliahidi kugawa mtaji huo juzi alipofanya kikao na vijana wenye taaluma mbalimbali katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kwa ajili ya kusikiliza kero zao.

Alisema mtaji huo unatokana na faida ambayo anapata kutokana na uwekezaji wake kwenye shule zake za Patrick Mission iliyopo jijini Dar es Salaam na Paradise Mission iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya.

Alisema msaada huo atagawa bila kujali itikadi za kisiasa wala ubaguzi wa aina yoyote na badala yake kuna vigezo vitaandaliwa vya kuwashindanisha mama lishe hao ili watakaoshinda ndio wapatiwe.

"Tuikimbize Mbeya Vijijini yetu na asiwepo wa kuzuia hili jambo tunahitaji kusonga mbele ndiyo sababu hapa nimeita vijana wa makundi yote kutoka kata zote bila kuangalia itikadi za vyama vyao kikubwa ninachotaka tuungane kwa pamoja kuijenga wilaya yetu," alisema Mwaselela.

Kwa upande wake Mjumbe wa Halmashauri Kuu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Kenneth Laulesi, alisema mikutano ya kusikiliza kero za wananchi inayofanywa na viongozi wa chama hicho mbali na kutatua kero hizo pia inasaidia kuwaunganisha wananchi.

Aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo, huku akisisitiza kwamba mkoa huo una fursa nyingi za kiuchumi ambazo vijana wakizichangamkia wanaweza kupata utajiri.

# Utafiti ndizi, magonjwa katika migomba waanza

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

SERIKALI imeanza kufanya utafiti shirikishi wa uzalishaji wa ndizi na namna ya kukabiliana na magonjwa ya migomba katika maeneo yenye ukame kwenye mikoa mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Utafiti huo unafanyika kwa ushirikiano kati ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) vituo vya Maluku cha mkoani Kagera na Kituo cha Uyole cha jijini Mbeya ambacho kinahudumia mikoa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Akizungumza wakati wa utafiti huo katika Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, mtafiti wa migomba kutoka Kituo cha Maluku, Joseph Kimisha alisema waliamua kuwashirikisha wakulima ili kuwapa nafasi ya kuchagua aina ya mbegu ambayo itafaa katika maeneo yao.

Alisema wanafanya utafiti wa mbegu mbalimbali na kwamba wakulima pia wanatoa maoni yao na kuchagua aina ya mbegu zitakazoleta tija kwenye maeneo yao.

"Tunawashirikisha wakulima kwa sababu wao ndio wazalishaji na wanatakiwa kutoa maoni yao ambayo yatatusaidia pia sisi kwenye kufanya uamuzi, hapa tuna aina mbalimbali za mbegu za ndizi ambazo tunazifanyia utafiti," alisema Kimisha.

Mtafiti kutoka TARI Uyole, Japhet Mdede alisema katika halmashauri hiyo ya Busokelo walifanya utafiti katika Kata ya Kisegese ambayo ina asili ya ukame hasa kipindi cha kiangazi na hivyo ni lazima wananchi watumie mbegu inayohimili hali hiyo.

Alisema walifanyia utafiti mbegu nyingi lakini ile ambayo wameipeleka kwa wakulima hao ni ile ambayo inahimili ukame na kukinzana na magonjwa mbalimbali ambayo yamekuwa yakishambulia migomba kwenye maeneo ya ukame.

"Lakini mbegu hizi tulizozichagua kwa ajili ya eneo hili zipo nyingi, sasa tunawashirikisha wananchi ili wachague aina wanayoitaka ili sasa waendelee kuitumia," alisema Mdede.

Baadhi wa wakulima ambao walishirikishwa kwenye utafiti huo walisema kwenye eneo hilo walianza kukata tamaa ya kuzalisha ndizi kutokana na hali ya hewa kutokuwa rafiki kwa zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Lusajo Mwatebela, alisema eneo hilo wamekuwa wakilima ndizi lakini hazistawi vizuri kutokana na hali ya ukame ambayo inalikumba eneo hilo.

Alisema miaka ya nyuma walikuwa wanazalisha ndizi lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi waliacha kuzalisha na sasa wameanza kupata matumaini ya kuanza tena.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Kisyegesya iliyopo Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Sosoma Zakalia alisema utafiti huo utasaidia kuongeza mwamko wa wananchi kulima ndizi.



## Utafiti waeleza chanzo w'biashara kukaidi kulipa kodi

**Na Mwandishi Wetu**

MTAALAMU wa masuala ya kodi kutoka Taasisi ya Kodi ya Norway (CMI), Profesa Odd-Helge Fjeldstad, amesema nchi nyingi za Afrika wafanyabiashara hawana imani na taasisi za kukusanya kodi, hivyo elimu ni miongoni mwa mbinu pekee zinazohitajika kurudisha imani.

Aliyasema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati akiwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu namna ya ulipaji wa kodi unavyoweza kuleta maendeleo ya biashara.

Hafla ya uwasilishaji wa utafiti huo ilihudhuriwa pia na watendaji wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na jumuiya za wafanyabiashara.

Prof. Fjeldstad alisema katika baadhi ya nchi wafanyabiashara wanaziona mamlaka za kukusanya kodi kama adui wa biashara zao.

Alieleza kuwa kukwepa kodi ni changamoto kubwa katika wajibu wa ulipaji kodi, ambapo utafiti unaonesha sheria na kanuni hazishughulikii vya kutosha ukwepaji kodi, hali inayoonesha iko haja kuijengea jamii uwezo na maarifa ili ikubaliane na wajibu wa kulipa kodi kwa hiari.

Profesa huyo ambaye ni msimamizi wa mradi wa miaka mitano unaohusu kuelimisha umma umuhimu wa kodi, alitaja mambo mawili kati ya maeneo waliyotafiti.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni kanuni zinazoathiri utayari na uwezo wa kulipa kodi pamoja na kuamini usimamizi, akisema maeneo hayo yanaweza kuwa muhimu kwa kuhamasisha umma kuhamasika kulipa kodi.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa uwezo wa serikali kukusanya kodi unategemea utayari wa watu kulipa, akisema kuhimiza utiifu wa kodi kunahitaji uelewa makini wa jinsi walipa kodi wanavyofikiri kuhusu uzoefu wa kutozwa ushuru.

Akifungua warsha hiyo, Kamishna wa ZRA, Juma Yussuph Mwenda, alisema pamoja na changamoto kadhaa, ufanisi katika ulipaji kodi nchini unaridhisha.

Alisema matokeo ya utafiti huo ambapo wafanyabiashara mbalimbali wa Zanzibar walifikiwa na kutoa maoni yao, yameonesha jinsi ZRA inavyoaminiwa na wateja wake.

Aliwataka wafanyabiashara kuongeza kasi ya kulipa kodi, pamoja na kuwa na amani kwani kodi zao zinatumika kwa manufaa ya wananchi wakiwamo wao wenyewe.

Alisema kila mwenye macho anaoina namna serikali inavyoimarisha sekta mbalimbali za maendeleo, ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, michezo, kuinua elimu, afya na huduma nyingine za jamii.

# Serikali yataja faida uwekezaji katika Bandari ya Malindi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Muhammed amesema tangu Serikali ya Zanzibar ilipoingia mkataba na Kampuni ya Afrika Global Logistic (AGL) ya uendeshaji wa Bandari ya Malindi faida lukuki zimepatikana mojawapo ni kudhibiti upotevu wa mapato.

Amesema faida nyingine ni kuimarika kwa operesheni za kutoa huduma za upakiaji na ushushaji wa mizigo bandarini.

Alitoa ufafanuzi huo wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe, aliyetaka kujua ni kwa kiasi gani lengo na dhamira iliyokusudiwa na serikali imekamilika tangu kubinafsishwa kwa bandari hiyo.

Akijibu swali hilo, Waziri Dk. Khalid alisema lengo na dhamira ya serikali imefikiwa, kwamba faida mbalimbali zinaendelea kupatikana hadi sasa ikiwamo kuimarika kwa operesheni za kutoa huduma za upakiaji na ushushaji wa mizigo bandarini.

Alitaja faida nyingine ni kudhibiti upotevu wa mapato, uingiaji na utokaji wa kiholela kwa wasiohusika na shughuli za bandari kwa lengo la kuimarisha hali ya usalama katika bandari hiyo, kuweka taa katika eneo la makontena.

Kadhalika alisema mafanikio mengine ni kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 41, kuendelea na ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Maruhubi yenye ukubwa wa hekta mbili ambapo ujenzi kwa sasa umefika zaidi ya asilimia 80, sambamba na kuongezeka kwa vitendea kazi vipya.

Akizungumzia tofauti ya kiutendaji ya utoaji wa makontena zamani na sasa, alisema inaonekana katika kuongezeka kwa uharaka wa ushushaji wa makontena ambapo kwa sasa bandari ina uwezo wa kutoa makontena 10 mpaka 12 kwa saa moja ikilinganishwa na kutoka makontena saba mpaka nane kwa saa moja kabla ya makubaliano hayo.

Alisema kwa sasa meli ya mizigo hupiga nanga kwa siku saba na siyo zaidi ya siku 15 kusubiria kupakua mizigo ambapo mwanzo ilikuwa zikisubiri kwa zaidi ya siku 20 hadi 30.

Aidha, alisema serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kuwa na matumaini chanya kwa wawekezaji ambapo hatua za matokeo mazuri zinaendelea kuonekana kwa wananchi pamoja na wafanyabiashara.

Pia, aliwataka wananchi na wafanyabiashara kuendelea kuzitumia Bandari ya Malindi na Fumba ili kurahisisha huduma za kuingiza na kusafirisha mizigo yao na biashara zao kwa lengo la kukuza uchumi na ustawi wa maisha kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi chini ya Shirika la Bandari iliingia mkataba na Kampuni ya Afrika Global Logistic (AGL) Mei 18 mwaka jana.



Mjumbe wa Kamati Kuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mansour Yussuf Himid, akizungumza jana katika mkutano wa chama hicho uliofanyika kiwanja cha Magogoni kwa Mabata Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matukio udhalilishaji watoto bado tatizo Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kipindi cha Mei mwaka huu matukio ya vitendo vya udhalilishaji visiwani Zanzibar 172 yaliripotiwa, huku mengi yakiwa ni ya watoto

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ramla Hassan Pandu, alitoa takwimu hizo wakati akiwasilisha takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa kipindi cha Mei mwaka huu.

Alisema miongoni mwa idadi hiyo, watoto walikuwa ni 143, wasichana walikuwa 111 sawa na asilimia 77.6 na wavulana walikuwa 32 sawa na asilimia 22.4.

Ramla alisema idadi ya matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 79 ambapo waathirika 70 walikuwa wasichana na tisa walikuwa wanawake na matukio ya kulawiti yalikuwa 15 ambapo waathirika wote walikuwa wavulana.

"Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni tisa ambapo waathirika wanane walikuwa ni wasichana na mmoja ni mwanamke," alisema.

Aliitaja Wilaya ya Mjini ndiyo iliyoongoza ikiwa na matukio 45 sawa na asilimia 26.2, ikifuatiwa na Magharibi 'A' iliyoripotiwa matukio 37 sawa na asilimia 21.5.

Alisema Wilaya ya Kaskazini 'A', Kusini na Micheweni ziliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio manne kwa kila wilaya sawa na asilimia 2.3.

Aidha, alisema idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 16.2 kwa kufikia matukio 172 kipindi cha Mei kutoka matukio 148 yaliripotiwa Aprili 2024.

Pia, alisema idadi ya matukio kwa mwaka pia yameongezeka kwa asilimia 11.7 kufikia 172 kipindi cha Mei 2024 kutoka matukio 154 kwa kipindi cha Aprili 2023.

Alisema jumla ya majalada 93 ya makosa ya udhalilishaji yalipokolewa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kipindi cha Mei, 2024, ambapo yalihusisha makosa 96 na idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yalitokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 59) sawa na asilimia 61.5 ya makosa yote ukilinganisha na mikoa mengine.

Alisema kati ya majalada 93 yaliyopokelewa 16 yalipendekezwa kufungwa, majalada 32 yalirudishwa polisi kwa upelelezi zaidi, majalada 27 yaliruhusiwa kwenda mahakamani na 18 hayajatolewa uamuzi.

Alisema miongoni mwa makosa 96 ya udhalilishaji yaliopokelewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliojitokeza yalihusiana na kubaka (makosa 54) sawa na asilimia 56.3 ya makosa yaliopokelewa.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee, Siti Abass Ali, alisema jamii na wazazi wanahitaji kujenga ushirikiano katika malezi ili kuendelea kupunguza vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo la udhalilishaji lililoshamiri kuna umuhimu kwa wanajamii kushirikiana, kila mmoja atapaswa kutoa ushirikiano ili kumaliza tatizo hilo.

Mkaguzi wa Polisi Dawati la Jinsia Makao Makuu ya Polisi, Makame Haji Haji, alisema ni vizuri kwa wazazi wakafuatilia nyendo za watoto wao kila siku tena kwa umakini ili kujua namna ya kuepusha vitendo vya udhalilishaji.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.
Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU
Shauri la Madai Na.59/2023

**Jina la Mdai:AGNES FEYA**
**Jina la Mdaiwa:NKUBA MASAKA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa:NKUBA MASAKA WA SANGAMWALUGESHA**

**K.K: VEO SANGAMWALUGESHA,MASWA.**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) Kugawana chumo la pamoja.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 28 Mwezi 06 Mwaka 2024 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa sharini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13Mwezi 06 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN BEN MATOWO** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki aina ya **FEKON** zenye usajili **MC 900 BQL** na **MC 525 BRV,** kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae.

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/TAN/TAN/6114/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAM STANSLAUS MUSHI a**natangaza kupotea kwa cheti cha **SHORT COURSE SECRETARIAL** kilichotolewa **CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA (TPSC) TAWI LA TANGA** mwaka **FEB.2019.** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/TAN/LUS/6079/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA ABDALLAH NGODA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0446-002** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MOROGORO SECONDARY SCHOOL**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: 9910841339571**

## KUPOTEA KWA TRANSCRIPT



**SAFINA MUSA MZIRAY** anatangaza kupotea kwa transcript yenye usajili namba **IRDP/TCCD/SEE22/0006** ya kozi ya **COMMUNITY DEVELOPMENT** iliyotolewa na **CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA PHQ/DOD/DOD/25725/2024.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
TANGA
MAOMBI YA UTEKELEZAJI NA. 12448 YA 2024
PAULO PARISIANO, SOKORIANO KIPALA NA WENZAKE 79 ....... WALETA MAOMBI
DHIDI YA
KWAMWANDE VILLAGE COUNCIL NA WENZAKE 49
.................... WAJIBU MAOMBI

**KWENDA KWA:-**
KWAMWANDE VILLAGE COUNCIL, ALLY OMARY MAGWADU (THE CHAIRMAN OF KWAMWANDE VILLAGE COUNCIL), MUYA JUMA, RAMADHANI JUMA, MSINDO SENGORI, MNGOYA JUMA, ALLY JUMA, HATIBU HOSENI, MOHAMEDI HOSENI, ATHUMANI HOSENI, OMARI SENGORI, AMIDI MUYA, NGIDO SANGAO, HASSANI MHANDO, MHANDO NYERERE, ALI HOSENI, MWEJUMA NASORO, MICHAEL MATHIAS, BAKARI SANGORA, BAKARI ABDALLAH, SAIDI BAKARI, CHAUYA KIFUNDA, SAIDI MHANDO, SANGORI CHAMBO, MR. KIVUMO, MR. MLOLWA, MNYAMISI SARIMU, MBWANA NASORO, MUYA JUMA MTAMBO, MNYAMISI HOSENI, LUKUWA MUYA, SOSERE KOMBO, MOHAMEDI MKERO, MBOTA SAIDI MADANGA, BAKARI MGANGA, SWALEHE MKAGIRA, MTAITA ATHUMANI, MWEJUMA MHIDINI, MUYA ALI, MBERWA BOTO, SALIMU SAKIBUJU, MBWANA KIMWERI, BAKARI HASSANI, JUMA NGORE, SANGARI SAMAGWADI, NYERERE NDALU, MBWANA MWANDE, SWALEHE MUSA, SWALEHE KILO na MR. JUSTIN.

**Popote Mlipo**

**KUITWA SHAURINI**

Waleta Maombi wamefungua shauri dhidi yenu mbele ya Mahakama Kuu ya Tanzania-Tanga. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 15/07/2024 saa 5:00 asubuhi mbele ya Mh. B. R. NYAKI, Naibu Msajili.
Hivyo basi mnatakiwa kuhudhuria nyinyi wenyewe au Wakili wenu kwa tarehe iliyopangwa bila kukosa. Endapo hamtahudhuria shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama Kuu ya Tanzania –Tanga leo tarehe 19/06/2024



JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Geita
Kituo cha Bulela Mkoa Geita
Shauri la Madai/ Ndoa Na.9/2024
Jina la mdai George Chacha Chongo
Jina la mdaiwa Ernest Mlezi Marithine wa Kasamwa-0644663188

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa Ernest Mlezi Marithine**
**Wa Kasamwa – 0655663188**
**Kwa kuwa mdai / wadai ameletea/ wameleta madai yake /yao kwamba (elezea habari za madai)**

Kujibu madai ya Tsh 500,000/= kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 mwezi 06 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 6 mwaka 2024



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA
Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa SIMIYU
Shauri la Madai Na 30/2024
Jina la mdai KCCL KAHAMA CO.LTD
Jina la Mdaiwa BENEDICTOR G. MAKUBI NA WENZAKE WANNE

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa EZEKIEL G.MAKUBI**
**WA MWASAYI**
**MASWA**
**K.K. M/KITONGOJI**
**MWAJIJABENDE**
**K.K VEO**
**MWASAYI**
**MASWA**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Mada Mdai anawadai wewe pamoja na wenzako wane pesa za ununuzi wa pamba

## KUPOTELEWA NA CHETI CHA CHUO



**SHEDRACK JUMA LUDOGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo cha Ualimu chenye index namba **E0603-0154** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia chuo cha **MUFINDI TEACHER'S COLLEGE** mwaka **2016**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.
**POLISI TAARIFA: PHQ/IRI/MUF/8775/2024**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA
Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa SIMIYU
Shauri la Madai Na 27/2024
Jina la mdai KCCL KAHAMA CO.LTD
Jina la Mdaiwa MISPINA KULWA NA WENZAKE WANNE

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanauni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa EMILY KULWA**
**WA BUGALAMA**
**MASWA**
**KK:M/KITONGOJI**
**BUGALAMA**
**KK:VEO**
**BUGALAMA-MASWA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Mda) Anawadai pesa sh.14,317,320/= ikiwa ni baki ya pesa za ununuzi wa pamba.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katiks Mahakama hii tarehe 18 Mwezi 6 Saa 2:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu ikithibitka kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusiskiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 Mwezi 06 Mwaka 2024.

KCBL KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED
Together, Transforming Lives

## TANGAZO

TUNAPENDA KUWAARIFU WENYEVITI NA WAJUMBE WA BODI WA VYAMA, MAKAMPUNI/TAASISI NA WANAHISA WOTE BINAFSI, KUWA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA SABA (27) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA USHIRIKA YA KILIMANJARO (KCBL), UTAFANYIKA SIKU YA IJUMAA, TAREHE 26 JULAI, 2024 KWENYE **UKUMBI WA GENERATION ULIOPO JIJINI DODOMA MAENEO YA KISASA,** KUANZIA SAA TATU (3:00) ASUBUHI.

TUNAPENDA KUWAKUMBUSHA KUWA KILA CHAMA/TAASISI/KAMPUNI ITUME **MJUMBE MMOJA TU,** NA MWANAHISA BINAFSI ANAYO NAFASI YA KUHUDHURIA BINAFSI AU KUWAKILISHWA KWA MUJIBU WA MASHARTI YA BENKI.

KARIBUNI SANA.

Godfrey J. Ng'urah,
**KATIBU-BODI YA WAKURUGENZI**

Tarehe: 19/06/2024

# CAREER OPPORTUNITY

The Guardian Limited, publishers of leading Tanzanian newspapers The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced professionals to fill the following position:

## Position: Sales Executive

**Job Purposes**
Sales Executive is responsible for driving advertising revenue by selling ad space in our newspapers to businesses, agencies, and other potential clients. This role involves building and maintaining relationships with clients, developing advertising strategies, and achieving sales targets.

**Key Responsibilities**

- Sell advertising space in our newspapers to new and existing clients.
- Develop and implement effective sales strategies to meet or exceed revenue targets.
- Build and maintain strong relationships with clients, understanding their business needs and advertising goals.
- Provide excellent customer service and support to ensure client satisfaction and retention.
- Work with clients to create customized advertising solutions that align with their marketing objectives.
- Stay informed about industry trends, competitor activities, and market conditions.
- Conduct market research to identify potential clients and new business opportunities.
- Maintain accurate records of sales activities, client interactions, and contracts in the CRM system.

**Other Responsibility**

- Develop and guide the team of freelancers.
- Assist and supervise freelancers through post-mortem meetings.
- Accompany freelancers on customer visits, analyze missed business opportunities, and create action plans.
- Monitor and evaluate the performance of freelancers, providing feedback and support for improvement.

**Qualification**

- Bachelor's degree in Marketing, Business Administration, Communications, or a related field.

**Experience:**

- Minimum of 2-3 years of experience in advertising sales, preferably in the media or publishing industry.
- Proven track record of meeting or exceeding sales target

Interested candidates who meet the above criteria should send in their applications enclosing a detailed CV addressed to the:

**HUMAN RESOURCES DEPARTMENT**
**THE GUARDIAN LIMITED**
**P.O.BOX 31042**
**DAR ES SALAAM – TANZANIA**
**OR email: vacancy@guardian.co.tz**
**DEADLINE: 29th June 2024. Only shortlisted candidates will be notified.**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Makabiliano washambuliaji na jeshi Russia yaua 19

**MOSCOW,** Russia

RUSSIA imesema makabiliano yaliyokuwa yakiendelea kati ya jeshi la nchi hiyo na washambuliaji yamemalizika huku yakisababisha vifo kwa Warussia 19, kati yao maofisa wa polisi wakiwa 15 na wananchi wa kawaida wanne.

Inaelezwa kuwa juzi usiku washambuliaji hao waliokuwa na silaha walivamia makanisa ya Orthodox na Sinagogi katika mji mkuu wa Dagestan, Derbent na katika kituo cha ukaguzi cha polisi, huku kamati ya kupambana na ugaidi katika taifa hilo ikibainisha kuwa washambuliaji watano wameangamizwa.

Ilielezwa kuwa haijabainika kwamba kuna washambuliaji wengine waliotoroka, huku sababu ya mashambulizi hayo ikiwa bado haijajulikana.

Msururu huu wa mashambulizi yanayoelezewa kama ya kigaidi na mamlaka ya Russia yanakuja miezi mitatu baada ya shambulio lililodaiwa kutekelezwa na kundi la wanajihadi la Islamic State (IS) lililofanywa katika ukumbi wa Crocus City, na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 140.

Aidha, ilielezwa kuwa Dagestan, eneo la Russia lenye waislamu wengi jirani na Chechnya, lilikuwa eneo la mapigano ya mara kwa mara ya wanajihadi katika miaka ya 2000, kama sehemu kubwa ya Caucasus. Na kwamba uasi huo ulikomeshwa na majeshi ya Russia baada ya miaka mingi ya mapigano. **RFI**

**Ilielezwa kuwa haijabainika kwamba kuna washambuliaji wengine waliotoroka, huku sababu ya mashambulizi hayo ikiwa bado haijajulikana.**

# Netanyahu: Vita Gaza karibuni kumalizika

**JERUSALEM,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amebainisha kwamba vita vya kutumia silaha vinavyoendeshwa na jeshi la taifa hilo dhidi ya wapiganaji wa Hamas katika mji wa Rafah, kusini mwa Ukanda wa Gaza, viko karibuni kumalizika.

Netanyahu aliyaeleza hayo jana katika mahojiano aliyofanyiwa na chombo kimoja cha habari cha Israel, ambako kwa mara ya kwanza tangu vita hivyo vianze ameonyesha matumaini ya kumaliza vita hivyo vilivyodumu kwa zaidi ya miezi saba.

"Hii haimaanishi kwamba vita vinakaribia kuisha, lakini vita katika awamu yake ya vurugu vinakaribia kumalizika huko Rafah," alisema.

"Tukimaliza vita na Hamas mjini Rafah tunaelekea Lebanon, tutapeleka baadhi ya vikosi vyetu kuelekea kaskazini, na tutafanya hivyo kwa madhumuni ya kujihami, lakini pia kurejesha wakazi waliofukuzwa kwenye makazi yao."

Netanyahu pia alisisitiza kwamba hatakubali makubaliano yoyote ya muda, na kwamba lengo ni kurejesha mateka na kuangusha utawala wa Hamas huko Ukanda wa Gaza.

Akijibu swali kuhusu hatima ya Gaza baada ya vita, Netanyahu alieleza kuwa Israel itakuwa na jukumu la kutekeleza kwa muda kupitia udhibiti wa kijeshi.

"Pia tunataka kuanzisha utawala wa kiraia, kwa ushirikiano na Wapalestina wa ndani ikiwezekana, na pengine kwa usaidizi wa nje kutoka nchi za kanda, ili kusimamia misaada ya kibinadamu na baadaye masuala ya kiraia katika Ukanda wa Gaza," alisema. **BBC**



Mmoja wa mahujaji waliokuwa wakishiriki ibada ya hija nchini Saudi Arabia, akiwa amekaa chini baada ya kuzidiwa na joto, huku serikali ya taifa hilo ikieleza kuwa zaidi ya watu 1,300 wamefariki baada ya kukabiliwa na joto kali wakati wa utekelezaji wa ibada hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# Maandamano wananchi Kenya, Rais Ruto atoa neno

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, amesema kwamba yuko tayari kufanya mazungumzo na maelfu ya vijana waliofanya maandamano kwa amani wiki iliyopita kwa lengo la kupinga mapendekezo ya nyongeza ya kodi.

Maandamano hayo yaliandaliwa kwenye mitandao ya kijamii na vijana Wakenya wengi wenye umri mdogo maarufu kama (Gen-Z) ambako wakati wa utekelezaji wake waliyarusha moja kwa moja kwenye mitandao ya kijamii.

Ilielezwa kuwa vijana hao wameendelea kuonyesha msisitizo juu ya kutoridhishwa na sera za kiuchumi za serikali ya Rais Ruto.

Ikiwa ni tamko lake la kwanza tangu kufanyika kwa maandamano hayo, Rais Ruto jana alisema "Ninajivunia sana vijana wetu, wamepiga hatua mbele kwa kufanya maandamano ya amani na ninataka kuwaambia kwamba tutawashirikisha."

Aliongeza kuwa serikali yake itafanya mazungumzo na vijana ili kwa pamoja walijenge taifa la Kenya liwe kubwa zaidi.

Aidha, licha ya kauli ya kiongozi wa taifa hilo bado upande wa waandaaji wa maandamano hayo ya kupinga ongezeko la kodi haujatoa majibu kama wanakubaliana na wito wa Rais Ruto au la huku wakiitisha maandamano mengine ya kitaifa leo.

Hata hivyo, pamoja na Rais Ruto kuyaita maandamano hayo kuwa ni ya amani, wanaharakati wa haki za binadamu wameripoti vifo vya waandamanaji wawili vilivyotokana na maandamano Alhamisi mjini Nairobi.

Ilielezwa kuwa maandamano hayo kwa kiwango kikubwa yalikuwa ya amani, lakini maofisa wa Jeshi la Polisi walirusha mabomu ya kutoa machozi na maji ya kuwasha kwa siku nzima ili kuwatawanya waandamanaji waliokuwa karibu na Bunge.

Kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya, kijana Evans Kiratu (21), alipigwa bomu la kutoa machozi wakati wa maandamano hayo na alifariki akiwa hospitalini.

Polisi ya Kenya ilisema inachunguza madai kukusu kupigwa risasi na maofisa wa polisi kijana mwenye umri wa miaka 29 jijini Nairobi baada ya maandamano hayo. Huku Mamlaka Huru ya Kusimamia Jeshi la Polisi nchini Kenya (IPOA) ikisema imeorodhesha kifo hicho kuwa ni matokeo ya kupigwa risasi na polisi.

Vile vile, mashirika kadhaa, likiwamo la 'Amnesty International Kenya' yalisema takriban watu 200 walijeruhiwa katika maandamano hayo yaliyohusishwa maelfu ya vijana walioingia barabarani kupinga mswada wa sheria ya kuongeza kodi Kenya.

Serikali ya Rais William Ruto inayokabiliwa na uhaba wa fedha ilikubali kufanya mabadiliko baada ya mamia ya waandamanaji vijana kukabiliana na polisi katika mji mkuu wa Kenya.

**KUHUSU KODI**

Pia serikali nchini humo umetetea mipango ya kuongeza kodi kwa kiwango cha dola bilioni 2.7 (Sh. trilioni 7) ili kupunguza nakisi ya bajeti nchini humo. Na kwamba nyongeza za kodi zilizopendekezwa zinahitajika ili kuijaza hazina yake na pia ni hatua itakayoisaidia Kenya kupunguza utegemezi wa kukopa kutoka nje.

Kenya ina mlima wa deni, na gharama za kushughulikia ulipaji wa madeni zimeongezeka kutokana na kushuka kwa thamani ya sarafu ya nchi hiyo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, hali inayoifanya serikali ya Rais Ruto kuwa kwenye kipindi kigumu.

Waandamanaji walisema ongezeko la kodi mpya zinazopendekezwa katika muswada wa sheria ya fedha, zitaathiri uchumi na zitaongeza gharama za maisha kwa Wakenya ambao tayari wanakabiliwa na hali ngumu.

Kenya ni mojawapo ya nchi zenye uchumi unaokua katika eneo la Afrika Mashariki lakini theluthi moja ya watu wake milioni 51.5 wanaishi katika umaskini. **DW**

**HABARI MICHEZO**

# CHIPUKIZI YAJITOA MICHUANO CAF, TIMU 2 ZAITAKA NAFASI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Chipukizi FC imeliandikia barua Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kuitaarifu rasmi kuwa haitoshiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika licha ya kuwa mabingwa wa Kombe la FA kwa msimu huu.

Chipukizi FC ilitawazwa kuwa bingwa wa kombe hilo la ZFF baada ya mchezo wa fainali ulioikutanisha na timu ya JKU SC kushindwa kumalizika kutokana na wachezaji na benchi la ufundi la JKU kumfanyia fujo mwamuzi wa mchezo huo na kusababisha mechi hiyo kuvunjika.

**Kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano hayo, Chipukizi FC ilitawazwa kuwa wa kombe hilo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alithibitisha kupokea barua hiyo na kusema sababu kubwa waliyoeleza katika barua hiyo ni ukata wa fedha unaowakabili.

Alisema barua hiyo ilieleza kuwa kutokuwa na fedha kutawapa wakati mgumu wa kushindwa kumudu gharama za kuishughulikia timu katika mashindano hayo makubwa kwa ngazi za klabu Afrika.

"Tumepokea barua yao ambayo kikubwa walichosema ni ukata wa fedha ambazo ndani yake zinahitajika kuiandaa timu, lakini pia gharama nyingine za maandalizi yote," alisema.

Aidha, Vuai alisema kulingana na Kanuni za CAF, ZFF imechukua hatua ya kuziandikia barua klabu zote za Ligi Kuu ambavyo vitakuwa na uwezo wa ushiriki wa mashindano hayo, lakini pia vilivyowahi kushiriki mashindano ya kimataifa kwa ngazi za klabu hapo awali.

Alisema klabu mbili ambazo ni Zimamoto SC pamoja na Uhamiaji FC, ndizo zimetoa jibu la kuitaka nafasi hiyo na tayari wamevituma CAF na kwamba timu ambavyo itakidhi vigezo ndio itakayokuwa mwakilishi wa Zanzibar katika michuano hiyo.

"Tulituma taarifa CAF na walitutaka kupelekea timu yoyote ya Ligi Kuu ambayo inauwezo wa kushiriki mashindano hayo, lakini pia iweze kufikia vigezo vya leseni za klabu, hivyo kati ya timu hizo mbili tunasubiri majibu ya CAF, ambayo itakidhi vigezo.

Hata hivyo, alisema kwa sasa hivi wanaendelea na utaratibu wa kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu hasa katika zoezi la leseni za klabu kwa timu zote za ligi hiyo.

## Uhamiaji yadai imefikia robo ya malengo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU ya Uhamiaji, imesema katika msimu uliomalizika wiki iliyopita, wamefikia robo ya malengo yao kwa kumaliza Ligi Kuu katika nafasi ya sita licha ya kwamba lengo lao kubwa lilikuwa kumaliza katika nafasi nne za juu.

Uhamiaji FC katika michezo 30 waliyocheza wamefanikiwa kushinda 12, sare 11 na kupoteza mechi saba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Salehe Abas Mohmed, alisema kwa ujumla msimu huu ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa ikilinganishwa na misimu iliyopita.

Alisema kwa upande wa timu yao, ingawa hawakutimiza lengo lao, lakini pia wamefanikiwa kwa kumaliza nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo iliyokuwa na timu 16.

Alisema changamoto kubwa iliyojitokeza katika msimu huu ni mabadiliko ya ratiba za mara kwa mara hasa kwa mzunguko wa lala salama hali iliyosababisha kuharibu hata mpangilio wa mazoezi wa kujiandaa na mchezo unaofuata.

Mohmed alisema ni vema katika msimu mpya wa Ligi Kuu, ZFF kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi kuangalia kwa makini suala la mabadiliko ya ratiba jambo ambalo muda mwingine linaweza kutia shaka na kuhusishwa na upangaji wa matokeo.

"Msimu huu ulitia fora kwa mabadiliko ya ratiba kila wakati, yaani mzunguko mmoja unaweza kubadilishwa hata mara tatu, utakuta sisi viongozi muda mwingine tunapata mashaka," alisema.

Hata hivyo, alisema sasa umefika wakati kwa ZFF kupitia Bodi ya Ligi kutoa ratiba ya msimu mzima wa ligi hiyo badala ya kutoa ratiba ya mzunguko mmoja ambao umekuwa na mabadiliko mengi.




Watoto wakifanya mazoezi ya mpira katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Timu ya Taifa ya Kuogelea yawika Kenya*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Mchezo wa Kuogelea imeshika nafasi ya tatu kati ya klabu zaidi ya 30 zilizoshiriki kwenye mashindano ya Taifa yaliyomalizika mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Nairobi, Kenya.

Timu hiyo imeundwa na wachezaji Crissa Dillip, Romeo Mwaipasi, Mark Tibarazwa pamoja na Delbert Kenemo.

Akizungumza na Nipashe moja kwa moja kutoka nchini Kenya, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi (pichani), aliwapongeza waogeleaji wake kwa kuweza kuipeperusha vema bendera ya Taifa.

"Haikuwa kazi rahisi kupata ushindi huu kwa kuwa tulikuwa tunashindana na klabu ambazo zimezoea kuogelea kwenye mabwawa ya mita 50 wakati sisi tumezoea kutumia ya mita 25," alisema Mwaipasi.

Alisema mbali na kupata nafasi hiyo, waogeleaji waliweza kufanya vema katika michezo yao ambapo Tibarazwa aliibuka mchezaji bora baada ya kupata medali tatu za shaba, mbili za fedha na mbili za dhahabu kwa vijana wenye umri wa miaka 14 na 15.

Kadhalika, Dillip alipata medali nane baada ya kufanya vizuri katika michezo yake yote kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 12 na 13.

Aliongeza kuwa Kenemo alivunja rekodi baada ya kufanikiwa kupunguza muda kwenye bwawa la mita 50 na kuibuka na medali ya dhahabu.

Kwa upande wa Mwaipasi aliibuka mchezaji bora kwa kupata medali ya fedha katika mbio moja, na medali ya fedha kwa mbio saba ambazo zote alifanya vizuri.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leordga Tenga, alieleza kufurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji hao kwenye mashindano ya watoto ya kuogelea yaliyokuwa yamefanyika kwenye bwawa la kuogelea lililopo katika Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST), Masaki, Dar es Salaam.

Tenga aliwapongeza wazazi kutokana na sapoti kubwa wanayowapa watoto wao kuhakikisha wanakuza vipaji vyao kupitia mchezo wa kuogelea.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GULER AFUATILIWA LIVER

LIVERPOOL inamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Uturuki mwenye umri wa miaka 19, Arda Guler kutoka Real Madrid. ***(Teamtalk)***

### CHALOBAH AWANIWA

KLABU ya Fulham imefufua nia yao ya kumnunua beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24, Trevoh Chalobah. ***(Standard)***

### UTD KUMTOSA BRANTHWAITE

KLABU ya Manchester United itaachana na mazungumzo na Everton kwa ajili ya kumnunua mlinzi, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, endapo The Toffees hawatapunguza bei yao ya pauni milioni 70. ***(ESPN)***

### YORO ANAITAKA MADRID

MLINZI wa Lille, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, anapendelea kuhamia Real Madrid badala ya Liverpool au Manchester United. ***(Marca)***

### KUDUS NA WEST HAM

KLABU ya West Ham inahofia winga wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye umri wa miaka 23, ataomba kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### SOULE AULIZIWA VILLA

ASTON Villa imeuliza kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Matias Soule mwenye umri wa miaka 21, lakini Juventus inasema hauzwi. ***(Sky Sports)***

### KADIOGLU AWINDA ARSENAL

ARSENAL imewasilisha ombi la kumnunua beki wa pembeni wa Fenerbahce, Ferdi Kadioglu, 24. ***(Ajan Spor)***

### ATAJWA CHELSEA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na Boca Juniors kuhusu dili la kumnunua beki wa Argentina mwenye umri wa miaka 19, Aaron Anselmino. ***(Athletic)***

### ZIRKZEE ANYATIWA MAN U

KLABU ya Manchester United inajiandaa kutumia kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 33.8 katika mkataba wa mshambuliaji wa Bologna, Mholanzi Joshua Zirkzee, 23. ***(Telegraph)***

### SIMONS ALENGWA BAYERN

KIUNGO wa kati wa Paris St-Germain na Uholanzi, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21, ndiye anayelengwa na Bayern Munich. ***(Bild)***

### PIOLI ANUKIA AL-ITTIHAD

KOCHA wa zamani wa AC Milan, Stefano Pioli, ni miongoni mwa wanaowania kuwa kocha wa Al-Ittihad. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KANE AJIBU SHUTUMA UCHEZAJI DUNI ENGLAND

**COLOGNE,** Ujerumani

NAHODHA wa England, Harry Kane, amejibu shutuma za Gary Lineker za uchezaji wa England katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Denmark kwenye michuano ya Euro 2024.

**Lineker, mchezaji wa zamani wa Kimataifa wa England na sasa mchambuzi wa matangazo ya BBC ya mashindano hayo, alikuwa ametaja uchezaji umbovu wa kikosi hicho.**

"Kuwajenga vijana kwa kujiamini ingekuwa njia bora ya kuishughulikia," alisema Kane katika mkutano na waandishi wa habari wa Uingereza Jumapili.

"Jambo la msingi ni kwamba hatujashinda mashindano yoyote kama taifa kwa muda mrefu, na wengi wa hawa wachezaji wa zamani ambao wanakosoa walikuwa sehemu ya kushindwa pia.

"Wanajua jinsi ilivyo ngumu. Siwezi kamwe kumdharau mchezaji yeyote wa zamani, ninachoweza kusema ni kukumbuka tu jinsi ilivyokuwa kuvaa shati na kwamba maneno yao yanasikilizwa.

"Sote tunataka kushinda mashindano makubwa, nina uhakika wanataka tushinde mashindano makubwa, kuwa msaada wowote itakuwa njia bora ya kulishughulikia."

> ●●● Hawa wachezaji wa zamani wanaokosoa nao walikuwa sehemu ya kushindwa...

Kufuatia mchezo dhidi ya Denmark Alhamisi kumekuwa na maswali kuhusu uwezo wa safu ya mbele ya England kufanya kazi pamoja. Kane alikiri kuwa bado hawajafanya vya kutosha lakini akasisitiza kuwa hakuna matatizo ya msingi.

"Nina uhusiano mzuri na wote Jude Bellingham, Phil Foden na Bukayo Saka, hatujafanya vema vya kutosha katika michezo miwili kuonesha bado," alisema.

Huku kukiwa na ukosoaji mkubwa wa timu ya England, Kane aliwataka mashabiki watulie na kusisitiza kuwa bora zaidi.

"Wakati wa mashindano tuunge mkono tu kisha baada ya mashindano unaweza kutuhukumu," alisema Kane.

"Wakati wa mashindano ni jukumu letu kama wachezaji kuifanya sawa, bila shaka watu watakuwa na maoni yao, lakini mwishowe ni sisi ambao hufanya maamuzi na kupata suluhisho."

England ipo kileleni mwa Kundi C ikiwa na pointi nne na watamenyana na Slovenia katika mchezo wao wa mwisho wa kundi leo Jumanne mjini Cologne.

## HABARI MICHEZO



# MBAPPE HANA UHAKIKA KURUDI DIMBANI EURO 2024

**DORTMUND,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, anaendelea kupata nafuu kutokana na pua yake iliyovunjika ingawa bado haina uhakika kama atacheza leo Jumanne katika mchezo wa mwisho wa kundi la timu yake kwenye Euro 2024, Kocha Didier Deschamps amesema.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Mbappe ana nia ya kucheza na anatafuta nafasi katika kikosi cha kwanza cha Ufaransa kwa mechi hiyo.

Deschamps alikataa kusema kama Mbappe atacheza dhidi ya Poland huko Dortmund, lakini akatoa habari za kutia moyo kwa wafuasi wake kuhusu kupona kwa nahodha wake, ambaye alivunjika pua Jumatatu iliyopita kwenye mechi yao ya kwanza dhidi ya Austria.

"Utaona awe anacheza au la, lakini kila kitu kinakwenda katika mwelekeo sahihi, anapata nafuu na michubuko inapungua kila siku, na atazoea mask yake," alisema Deschamps.

TIMU ya matibabu ya Ufaransa wamefurahishwa na kuunganishwa kwa mfupa wa pua yake.

Kutokana na suluhu dhidi ya Uholanzi mjini Leipzig Ijumaa, wakati Mbappe alikaa kwenye benchi, kumekuwa na uchambuzi mwingi kwenye vyombo vya habari vya Ufaransa kuhusu uhodari wa kushambulia wa timu hiyo.

Bao pekee la Ufaransa katika mechi zao tatu zilizopita lilikuwa ni la kujifunga la Maximilan Wober wa Austria katika mechi yao ya kwanza ya Kundi D mjini Duesseldorf.

Lakini Deschamps hakujibu chochote alipoulizwa kama anaweza kufufua mashambulizi, hasa kwa vile Ufaransa, yenye pointi nne, inaonekana kuwa na uhakika wa kutinga katika hatua ya 16 bora.

# Kocha wa Brazil ataka uvumilivu kwa Endrick



**ATLANTA,** Marekani

KOCHA wa Brazil, Dorival Junior, alitoa wito wa "uvumilivu kidogo" kwa mshambuliaji Endrick mwenye umri wa miaka 17, baada ya kufichua kwamba usajili huo mpya wa Real Madrid hangeanza mechi yao ya kwanza ya Copa America dhidi ya Costa Rica Jana.

Endrick alifunga bao la ushindi kwa Brazil katika ushindi wa 1-0 wa kirafiki dhidi ya England kwenye Uwanja wa Wembley Machi mwaka huu, akafunga jingine katika sare ya 3-3 dhidi ya Hispania Uwanja wa Santiago Bernabeu na kuipa timu yake ushindi wa mabao 3-2 dakika za mwisho dhidi ya Mexico Juni 8 katika maandalizi ya Copa America.

Pia alikabidhiwa jezi maarufu nambari 9 kwa ajili ya mashindano hayo na kupendekeza jukumu kubwa kwa washindi hao mara tisa.

"Lazima uwe na subira kidogo," alisema Dorival akiwaambia waandishi wa habari Jumapili. "Ni kitu ambacho kitatokea kwa kawaida. Huenda isichukue muda mrefu kwa sababu ana ustadi mkubwa.

"Nina haraka ya kumwingiza uwanjani, lakini lazima uwe na uwiano fulani. Ana ujuzi bora na ni mmoja wa wachezaji wanaotegemewa."

Kocha huyo alitangaza kikosi cha kwanza ambacho kina wachezaji watatu wa mbele Raphinha pamoja na wachezaji wenzake wapya wa Endrick wa Real Madrid, Vinicius Junior na Rodrygo.

Pia inajumuisha nyuso mbili mpya, beki wa kati wa Real Madrid Eder Militão na beki wa pembeni wa Atletico Mineiro Guilherme Arana.

"Kikosi cha kuanzia kitakuwa na Militao na Arana," Dorival alisema. "Katika kila mchezo, ikibidi, kutakuwa na mabadiliko moja au mawili. Wachezaji wote wako tayari. Hakuna hata mmoja wao aliye chini ya matarajio yetu. Tumejiandaa kwa hali yoyote."

Dorival alibainisha usawa na uthabiti kama funguo za mafanikio mbele ya Brazil kuanza Copa Amerika katika Uwanja wa SoFi huko Inglewood, California.

Brazil pia itamenyana na Colombia na Paraguay katika Kundi D.

# Bayern wamalizana na Olise

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich inajipanga kumsajili Michael Olise baada ya kukubaliana ada ya uhamisho na Crystal Palace kwa ajili ya winga huyo.

Timu hiyo ya Bundesliga imefikia makubaliano yenye thamani ya pauni milioni 50.7 ikiwa ni pamoja na nyongeza ya kumkaribisha Olise Allianz Arena baada ya Chelsea kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania saini yake.

Mfaransa huyo hapo awali alivutia vigogo kadhaa wa Ulaya - ikiwa ni pamoja na Newcastle United - lakini sasa yuko mbioni kujiunga na timu ya Vincent Kompany.

Kulingana na ripoti kutoka Sky Sports, uhamisho wa Olise kwenda Bayern sasa unaonekana kuwa mzuri na anatarajiwa kusaini mkataba ambao utamfanya abaki Ujerumani hadi 2029.

Olise anaonekana kuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa katika enzi mpya ya Kompany kwenye Bundesliga na baada ya kuachwa kwenye kikosi cha Didier Deschamps cha Euro 2024.

Lakini alijumuishwa katika orodha ya kikosi cha nchi hiyo kwa Olimpiki ya majira ya joto.

Nyota huyo wa Palace alihamia London Kusini katika msimu wa majira ya joto wa 2021 na kusajili mabao kumi katika mechi 19 katika msimu wa 2023/24 ulioathiriwa na majeraha.

Mustakabali wa Olise katika Klabu ya Bayern umeifanya Chelsea kufikiria upya chaguo lao kwenye winga, huku Omari Kellyman wa Aston Villa akikaribia kuhamia Stamford Bridge, kama alivyosema mwandishi Fabrizio Romano.



HABARI MICHEZO

## Yanga yaisubiri

INATOKA UKURASA 24

ya klabu. Wanachama na mashabiki wa Simba subirini, msiwe na mashaka tutafahamu mbivu na mbichi," alisema.

Jana kwenye mtandao wake wa instagram, amewaambia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa ili nyumba ijengwe ni lazima kwanza ibomolewe.

"Msishtuke kuona nyumba yenu inabomolewa ili ijengwe mpya, imara na nzuri zaidi," aliandika Ahmed.

Taarifa zingine zilizopatikana kutoka vyanzo ndani ya Klabu ya Simba zinasema bado viongozi wa klabu hiyo wanahaha kumbakisha na wanaendelea na mazungumzo kwa siku hizi zilizobaki na yamefikia mahala pazuri.

"Hao wataendelea kumsajili kama ambavyo tumezoea. Ahmed anaongea taarifa rasmi ambazo mpaka apewe na viongozi na bado hajazipata, ila Chama ataendelea kuvaa jezi za Simba, watangoja 'thank you ' ya Chama watasubiri sana," alisema mtoa taarifa.

## Simba yavujisha

INATOKA UKURASA 24

Simba ikafanya naye mazungumzo ambayo yanaelezwa kufanikiwa.

Alipuuzia tetesi za kuondoka kwa beki Fondoh Che Malone, ikitajwa kuwa amepata ofa kwenye Klabu ya Kasimpasa FC ya Uturuki.

"Che Malone haendi popote, bado ni mchezaji wa Simba, ana mkataba na hatuwezi kumruhusu kuondoka kwa sababu tuna mipango naye," alisema.

Klabu ya Simba pia imetangaza rasmi urejeo wa winga wake iliyomsajili mwanzoni mwa msimu uliopita, lakini haikumtumia kutokana na majeraha ya muda mrefu, Kramo.

Winga huyo na kiungo mshambuliaji alisajiliwa kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast, alicheza mechi tamasha la Simba Day kati ya timu yake na Power Dynamos, Agosti 6, mwaka jana akiingia kutokea benchi, lakini baada ya hapo aliandamwa na majeraha yaliyowalazimu mabosi wa klabu hiyo kukata jina lake kwenye orodha ya wachezaji wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika na kuwekwa mwingine wa kigeni, huku akiendelea kupata mshahara na stahiki zake kama kawaida.

"Kramo alikuwa majeruhi karibuni msimu mzima, tumemtibu mwanzo hadi mwisho, huku tukimlipa stahiki zake zote hili inafaa tujipongeze, kwa sasa kijana amepona kabisa, tutakapokwenda kuweka kambi nchini Misri mwanzoni mwa mwezi wa saba atakuwa sehemu ya wachezaji wataokwenda kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao. Muda wa Wanasimba kumtazama na kumfaidi Kramo sasa umefika," alisema Ahmed.

# MASHUJAA FC YAMNASA RASMI KARIHE WA MTIBWA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kutajwa kutaka kumsajili Denis Nkane wa Yanga, Klabu ya Mashujaa FC imekamilisha usajili wa straika wa Mtibwa Sugar, Seif Abdallah Karihe, kwa mkataba wa mwaka mmoja.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa Karihe amesajiliwa kuziba pengo la Adam Adam ambaye ametimkia Azam FC na kutangazwa rasmi kama ni mchezaji wa timu hiyo kwa msimu ujao.**

Mtoa taarifa amesema usajili wa Karihe haukuwa na tatizo sana kwa sababu tayari klabu yake imeshuka daraja, lakini yeye mwenyewe akiwa katika ubora wa hali ya juu, hivyo pande zote mbili zilikuwa zinahitajiana.

"Tayari Karihe amepewa mkataba wa mwaka mmoja utakaomalizika 2025, kilichobakia ni kutangazwa rasmi tu, lakini haiwezekani kufanya hivyo mpaka tutakapomaliza usajili wote ndiyo tutaanza kutupia mchezaji mmoja mmoja kwenye ukurasa wa mitandao yetu ya kijamii," alisema mtoa habari wetu.

Siku chache zilizopita, mtoa taarifa hiyo alilipenyezea taarifa gazeti hili kuwa klabu hiyo iko kwenye mazungumzo na winga wa Yanga, Nkane ambaye amekuwa hapati nafasi kwenye kikosi hicho.

Alisema Nkane anamaliza mkataba wake wa miaka miwili na Yanga kwani alijiunga 2022 akitokea Biashara United ya Mara.

"Nilikwambia kuhusu Nkane, huyu dili halijakamilika kwa sababu kuna klabu zingine zinamhitaji, unajua mchezaji ambaye anatakiwa sana, hawezi kusaini haraka, anaangalia wapi wataweka pesa nyingi, hilo ndilo linatukwamisha," alisema mtoa taarifa huyo.

Nkane anatajwa kwenda kuchukua nafasi ya Omari Abdallah Omari, ambaye taarifa zinadai amesajiliwa na Klabu ya Simba.

Mtoa taarifa huyo alisema maandalizi yote ya msimu ujao yanaelekea kukamilika, ikiwamo suala la usajili na Ijumaa ijayo, wanatarajia kukwea boti kwenda Zanzibar kwa ajili ya kupiga kambi, tayari kwa kujiandaa na Ligi Kuu msimu wa 2024/25.

"Tarehe 28 mwezi huu tunategemea kuanza maandalizi ya msimu ujao 'pre-season' mjini Zanzibar, tukiwa na wachezaji wetu wote na ndiyo utakuwa wakati wa kuanza kuwatangaza," alisema.

HATARI...



Kipa wa Uswisi, Yann Sommer na beki wa kati wa timu hiyo, Fabian Schär, wakiwa katika harakati za kuondosha hatari katika lango lao kwenye mechi ya Kundi A ya Euro 2024 dhidi ya wenyeji wa michuano hiyo, Ujerumani, ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# *Coastal kambini mapema Julai*

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Klabu ya Coastal Union umesema utaingiza kambini mwanzo mwa Julai kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kimataifa pamoja na yale ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Steven Mguto, alisema malengo yao ni kufanya vema katika mashindano hayo kwa kusajili wachezaji watakaoongeza ushindani.

"Tutaanza kambi mapema kwa ajili ya kujiandaa na mashindano hayo, malengo yetu ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kimataifa," alisema Mguto.

Alisema msimu uliopita ulikuwa na ushindani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu kuhakikisha hazishuki daraja.

Mgutoa alisema msimu ujao unatarajiwa kuwa na ushindani zaidi, hivyo kunahitaji kujipanga kikamilifu na kuwataka mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono kama walivyofanya msimu uliopita.

"Ninaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano kama walivyotufanyia msimu uliopita ili tuweze kutimiza malengo yetu," alisema Mwenyekiti huyo.

Aidha, aliwataka wachezaji wasibweteke kipindi hiki cha mapumziko na badala yake waendelee kufanya mazoezi ili wazidi kuimarisha miili yao.

# Michezo

Jumanne Juni 25, 2024

Nipashe




## Bayern wamalizana na Olise

UKURASA 22

UTANIUA...



Beki wa kati wa Ujerumani, Jonathan Tah, akimchezea madhambi mshambuliaji wa Uswisi, Breel Embolo, kwenye mechi ya Kundi A ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa nchini Ujerumani juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC YAISUBIRI SIMBA DILI LA CHAMA

### ●●● Mbivu mbichi kujulikana Julai Mosi siku ambayo mkataba wake...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga inatarajia kuingia rasmi mkataba na kiungo mshambuliaji Clatous Chama Juni 30, mwaka huu na kutangazwa Julai Mosi, sababu kubwa ikielezwa kuisubiri Simba.

**Pamoja na Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, kudai kuwa mchezaji huyo amemaliza mkataba, lakini taarifa zinaeleza kuwa unamalizika Juni 30, mwaka huu na ndipo atakuwa kwenye wakati mzuri wa kusaini Klabu ya Yanga kama walivyokubaliana.**

"Kelele zote hizi bado Chama hajasaini mkataba na Yanga, ila makubaliano kati ya pande zote mbili yalifikiwa tangu Januari mwaka huu, mkataba unatarajiwa kusainiwa Juni 30, na inawezekana atatangazwa kuanzia Julai Mosi, katika Klabu ya Yanga, atakuwa ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi ukiondoa Stephane Aziz Ki," kilisema chanzo kutoka ndani ya Klabu ya Yanga.

Chanzo hicho kimesema Yanga imeshindwa kumsainisha mkataba rasmi na kumtangaza mapema kwa hofu kuwa tarehe ya kumalizika kwa mkataba na klabu yake haijamalizika, na hawataki kuingia matatizoni.

"Kama Simba wangekuwa wamempa barua ya kuagana naye sawa, lakini kwa sababu hawajampa, hawawezi kufanya hivyo," alisema mtoa taarifa wetu.

Maneno haya yanafanana na aliyosema, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, akidai wanachelewa kutangaza walioachwa na watakaosajili kuwa kutokana na baadhi ya klabu kuchelewa kuwapa barua ya kuachana na wachezaji wao kwa hofu ya kuhamia kwao.

"Kuna mchezaji mmoja anamaliza mkataba, lakini jamaa hawataki kumpa barua, wana hofu atakuja kwetu, wampe tu kijana wa watu ili aje kwenye klabu ya ndoto yake, na hilo ndilo limetufanya mpaka sasa tuahirishe au tuchelewe kuwapa 'thank you' tutakaoachana nao na kutangaza wachezaji ambao tumewasajili, lakini tutaanza kufanya hivyo Julai Mosi," alisema Kamwe siku chache zilizopita bila kutaja jina la mchezaji.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed, alisema mkataba wa Chama na Simba umemalizika.

"Niseme tu kuwa Chama amemaliza mkataba wake ndani ya Simba, hivyo ndivyo ninavyofahamu, sasa anaongeza, haongezi, tuwape nafasi viongozi wetu wanaoshughulika nalo, wakishakuwa kwenye nafasi nzuri watatuambia nini kimetokea, watanieleza niwaambie kitu gani kinaendelea.

"Chochote kitakachofanyika ni kwa maslahi ya Simba, maamuzi yatakayoamuliwa yatakuwa kwa maslahi ya klabu, hapa tunachoangalia ni namna gani timu inaweza kusonga mbele, tukiamua abaki, aondoke itakuwa ni kwa maslahi

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba SC yavujisha usajili, Kramo naye ndani

**Na Adam Fungamwango**

ZILE tetesi za usajili za Klabu ya Simba kupata saini za baadhi ya wachezaji akiwamo Elie Mpanzu kutoka Klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Yusuph Kagoma wa Singida Black Stars, zinaelekea kukamilika baada ya Meneja Habari na Mawasiliano wa miamba hiyo, Ahmed Ally, kugusia usajili wao, huku akitangaza rasmi kuwa winga wa klabu hiyo aliyekuwa majeruhi kwa muda mrefu, Aubin Kramo, amepona na yupo tayari kwa msimu mpya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ahmed alisema Mpanzu na Kagoma ni wachezaji wazuri wenye hadhi ya kuichezea Klabu ya Simba, huku akiwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa na subira kwani siku si nyingi wataweka wazi majina ya wachezaji wote waliosajiliwa pamoja na benchi la ufundi.

"Mpanzu, ni mchezaji mzuri mwenye hadhi ya kucheza klabu kubwa kama Simba, anakuja au haji ni jambo la kusubiri, hivi karibuni tu kila kitu kitafahamika," alisema Ahmed.

Winga huyo wa kulia ni mmoja wa wachezaji wanaotajwa kuwa watatua Msimbazi kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho ambacho ni kama kinaanza kujengwa upya baada ya anguko kuu msimu uliomalizika.

Akimzungumzia Kagoma, alisema huu ndiyo muda wake sahihi wa kwenda kwenye klabu hiyo.

"Kagoma, kiungo mkabaji wa maana sana, ana kipaji kikubwa, kwa sasa ni mchezaji wa Singida Black Stars, tusubiri kwanza, eneo letu la kiungo mkabaji lina mashaka sana kwa siku za hivi karibuni, kama anatua naamini kwa ubora aliyokuwa nao, atatusaidia sana, ni muda wake sahihi wa kuja Unyamani," alisema Meneja habari huyo ikionyesha tetesi hizo zinaelekea kukamilika.

Awali, ilitajwa kuwa mchezaji huyo angetua Klabu ya Yanga, lakini ghafla kibao kiligeuka na

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >